# Nipashe

Alhamisi Julai 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580642

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**ama** AFYA NA MAZINGIRA







## Ufuatiliaji kinga Corona sasa unavyopamba moto serikalini



UKURASA 11

**Wastaafu** wapewa angalizo mikopo umiza, biashara

UKURASA 4



**Waziri** aonya corona wasafiri, wasafirishaji

UKURASA 5

# Chanjo ya corona yawatia matatani

UK. 2

**Wadaiwa** kughushi vyeti, wizara yasema hali si shwari... *UK. 2 & 17...*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### ANAYEDAIWA KUUA MWANAWE AUAWA

MKAZI wa Kitongoji cha Kaloleni Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Alon Cardius (27), ameuawa kwa kipigo kutoka kwa wananchi wanaodaiwa kuwa wenye hasira kali baada ya kutuhumiwa kumuua mtoto wake kwa kumkata panga.

## Msajili na CHADEMA watunishiana misuli

UKURASA 5



KIKWETE

“Nilipogombea mwaka 2005 alinisapoti kikwelikweli. Nikiwa Rais alinipa ujasiri na ushauri”





OBASANJO

“Mkapa alitoa mchango mkubwa katika kuipata Afrika mpya na kupambana na VVU”

CLINTON

“Nilijivunia kufanya kazi na Rais Mkapa nilipokuwa Rais wa Marekani. Alikuwa na mtazamo uliolenga kuokoa maisha”



SAMIA

“Mkapa alikaribisha uwekezaji kutoka nje kwa kutumia diplomasia yake. Deni la Taifa alilipunguza kwa takriban nusu"

TONY BLAIR



“Alikuwa mzalendo wa kweli, kiongozi mpenda watu na mpigania mabadiliko na maendeleo ya kweli kupitia utandawazi”

# Vigogo walivyoguswa na utashi wa Mkapa

UK. 2


MICHEZO NI VITA YA KUSALIA, HESHIMA LIGI KUU UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Rais Samia: Chanjo inakuja

Na Mary Geofrey

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali iko katika hatua za mwisho kuagiza chanjo ya corona kwa ajili ya kujikinga dhidi ya maambukizi.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam alipozindua kogamano la Kumbukizi ya Hayati Benjamin Mkapa, lililoandaliwa na Taasisi ya Mkapa.

Rais Samia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo kwa kufuata maelekezo yote ya wataalamu wa afya kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba.

"Mwelekeo ni kwamba kila atakayehitaji chanjo iwe inapatikana na kama nilivyosema kabla kuwa chanjo hiyo ni ya hiari, hivyo basi ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba wadau wa afya kuunga mkono juhudi hizi za serikali," alisema.

Wakati Rais Samia akitoa rai hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, akizungumzia mwenendo wa ugonjwa huo, alisema jana kuwa tayari wameshaagiza chanjo na zinatarajiwa kuingia nchini ndani ya miezi mitatu au minne ijayo.

"Sisi tumeshaomba na kuagiza chanjo, tumeomba chanjo 'COVAX Facility' za aina mbalimbali ili kumpa uhuru mwananchi kuchagua, zipo chanjo za aina nne.

"Ndani ya miezi mitatu au minne tutakuwa tumeshapazipata na serikali inafanya juhudi zingine za kuzipata mapema zaidi," alisema Prof. Makubi.

Alifafanua kuwa chanjo itaanza kutolewa kwa watu walio kwenye hatari ya kuambukizwa kama watumishi wa afya, wanaokwenda kuhiji, wenye ulazima na wanaosafiri mara kwa mara na wameshatoa mwongozo wa kuratibu chanjo hizo.

Alimshukuru Rais Samia kwa namna anavyoshughulikia suala hilo, akiwaomba Watanzania kumuunga mkono.

"Serikali tumekuwa tukiendelea kukidhibiti ugonjwa wa corona, kwani wapo majirani zetu wameshaingia 'wave' (wimbi) la nne," alisema Prof. Makubi.

VIFO VIPO

Prof. Makumbi alidokeza kuwa maambukizi bado yapo kwenye baadhi ya mikoa, hivyo wanaendelea kudhibiti.

"Tunapaswa kuendelea kudhibiti maambukizi, vifo vipo, si kwa kiwango kikubwa lakini hakuna haja ya kuwa na hofu kwani tutaendelea kuishi na Covid-19 na cha muhimu ni kupambana nao kwa kunzigatia kinga," alisema Prof. Makubi.

Aliwataka wananchi kuendelea kujikinga na corona kwa kuendelea kunawa mikono kwa majisafi tiririka au vipukusi (sanitazer), kufanya mazoezi, kula lishe bora na bila kusahau matumizi ya tiba asili.

"Wizara tuendelee kutoa elimu kwani upo upotoshaji mkubwa kwa jamii kuhusiana na ugonjwa huu na njia za kukabiliana nao," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, Wilson Malosha, alisema wanaendelea kufuata mwongozo uliotolewa wa kujikinga na maambukizi kwa kunawa mikono kwa maji safi tiririka na sabuni, vipukusi au kuweka nafasi kati ya mtu na mtu kwenye maduka madogo na makubwa, baa na hoteli.



Rais Samia Suluhu Hassan, akikabidhi tuzo ya picha kwa Mama Anna Mkapa kwa kutambua mchango mkubwa wa Hayati Mzee Benjamin William Mkapa alioutoa kwa taifa, wakati wa kumbukizi ya mwaka mmoja tangu kufariki kwake, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Vigogo walivyoguswa na ujasiri wa Mkapa

Na Waandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Benjamin Mkapa, ameacha historia katika Taifa la Tanzania hatosahaulika kutokana na alivyosimamia majukumu ya kiuchumi na kutoa fursa kubwa ya uwekezaji kwa Sekta Binafsi.

Amesema Hayati Mkapa alifanya mageuzi makubwa katika uchumi na kuongeza mapato ya nchi kutoka Sh. bilioni 331.2 mwaka 1995 hadi Sh. trilioni mbili mwaka 2005 na kupunguza Deni la Taifa kwa takriban asilimia 50.

Rais Samia aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam katika kongamano la Kumbukizi ya Hayati Benjamin Mkapa, lililoandaliwa na Taasisi ya Mkapa na kushirikisha marais wastaafu wa ndani na nje ya nchi walioshiriki kwa njia ya mtandao.

"Nilibahatika kumfahamu Hayati Mkapa, alikuwa mtu wa kipekee sana. Mara kadhaa nilipopata fursa ya kukutana naye, utaondoka ukiwa na maarifa mengi.

"Alikuwa mwenye haiba ya mamlaka na kujiamini, busara na amejidhihirisha kwenye maandiko yake mengi.

"Alikaribisha uwekezaji kutoka nje kwa kutumia diplomasia yake, Deni la Taifa alilipunguza kwa takriban nusu," alisifu.

Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, akimwelezea Mkapa, alisema amemfahamu kwa takribani miongo minne kabla ya kuwa Rais hadi alipostaafu, akimtaja kwamba alikuwa shujaa na mwalimu wake.

"Mkapa alikuwa mwalimu wangu, kaka yangu, nilifanya naye kazi... kufurahia maisha yake na kuyaishi ni jambo jema, hii inatukumbusha kwamba ni muhimu kufanya hili," alisema.

Kikwete alisema kuwa Mkapa alipochaguliwa kuwa Rais kwa awamu zote mbili, alimchagua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje kwa miaka 10 na kipindi hicho kilimfanya afanye kazi naye kwa ukaribu zaidi hasa katika masuala ya kimataifa.

"Nilipogombea mwaka 2005, alinisapoti, kikwelikweli, nikiwa Rais alinipa ujasiri na ushauri. Katika maisha yote katika utumishi wa umma, akiwa mwandishi, balozi, mbunge, waziri na Rais, alitambua wananchi ni kipaumbele kwake, alikuwa mwenye maono na mchapakazi katika kusoma na kuandaa hotuba kwa umahiri," alisifu.

Kikwete alisema Mkapa alikuwa na hamu ya Afrika kuwa kubwa na kutimiza ndoto zake.

"Alianzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mkapa alianzisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na kuanzisha TACAIDS, MKUKUTA na TASAF.

"Kupitia taasisi yake, tutaendelea kuenzi maisha yake na kuyaishi. Mungu ampe pumziko la milele," alisema Kikwete.

**BILL CLINTON**

Rais wa zamani wa Marekani, Bill Clinton, alisema alijivunia kufanya kazi na Mkapa, akikumbusha kuwa walishirikiana katika masuala mengi hususan kuboresha afya.

"Rais wakati tukisherehekea maisha ya Benjamin Mkapa, ninapenda kutoa salamu za rambirambi kwa Watanzania kwa kupoteza marais wawili, John Magufuli na Benjamin Mkapa, kwa kipindi cha mwaka mmoja.

"Kipindi cha uongozi wangu kama Rais wa Marekani, nilijivunia kufanya kazi na Rais Mkapa. Katika shughuli za afya mwaka 2002, alinialika kushiriki mradi ambao ulilenga kuokoa maelfu ya Watanzania dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) pamoja na malaria, mtazamo wake ulilenga kuokoa maisha," alisema Clinton.

**OBASANJO**

Rais wa zamani wa Nigeria, Olusegun Obasanjo, alisema alimfahamu Mkapa baada ya kupata nafasi ya kufanya naye kazi, akimsifu kuwa ni shujaa wa kuunganisha Waafrika.

"Tulifanya kazi pamoja NEPAD, AU, alitoa mchango mkubwa katika kuipata Afrika mpya na kupambana na VVU.

"Afrika imepoteza shujaa ambaye alikuwa mpigania haki na mpambanaji kuondoa kila aina ya ubaguzi kusini mwa Afrika.

"Nilimpigia simu mara kadhaa na kutoa ushauri kuhusu Afrika, ninamkumbuka katika mikutano yote tuliyokuwa pamoja," alisema Obasanjo.

TONY BLAIR

Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Tony Blair, alisema Mkapa alipenda nchi yake na Afrika kwa ujumla, akilenga kujikwamua na kupiga hatua za maendeleo.

"Ninafahamu alipo anajivunia sana kuona namna Taasisi ya Benjamin Mkapa inavyofanya kazi kwa niaba yake,"

"Mkapa ni kati ya vitu ninavyovithamini sana katika maisha yangu, imani yangu watu wote waliomfahamu walifurahia kufanya naye kazi, alikuwa mtu mwema na mwenye mtazamo," alisema Tony Blair.

**•Imeandaliwa na Christina Mwakangale na Anaeli Mbise**

## TANGAZO

# TAARIFA KWA UMMA

**Kufuatia marekebesho yaliyofanywa na serikali kupita sheria ya fedha ya mwaka 2021 na kwenye kifungu namba 46A (2) cha sheria ya Mfumo wa Malipo wa Taifa (National Payment Systems), Waziri wa Fedha kwa kushirikiana na Waziri wa Mawasiliano wamepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni zitakazosimamia namna ya ukusanyaji wa tozo za serikali kwenye miamala ya kutuma na kutoa fedha kwa njia ya simu. Kanuni zimetolewa na Waziri wa Fedha kwa kupitia Notisi ya Serikali namba 496A iliyochapishwa tarehe 30 Juni 2021. Kufuatia marekebisho haya ya sheria, kampuni ya Tigo Pesa itaanza kukusanya tozo hizo kwa niaba ya serikali kuanzia tarehe 15 Julai 2021.**

***Lifuatalo ni jedwali linalonyesha aina ya tozo mbalimbali zitakazo tozwa kwa watumiaji wa simu kulingana na kiwango cha miamala itakayofanyika.***


tigo pesa

## Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | | | Kutuma pesa kwenda mitandao washirika | | | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | - | 15 | 15 | - | 15 | - | - | - |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 10 | 40 | 50 | 10 | 60 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 16 | 46 | 50 | 16 | 66 | 400 | 16 | 416 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 27 | 77 | 100 | 27 | 127 | 600 | 27 | 627 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 56 | 116 | 100 | 56 | 156 | 650 | 56 | 706 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 100 | 230 | 200 | 100 | 300 | 950 | 100 | 1,050 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 125 | 275 | 200 | 125 | 325 | 1,000 | 125 | 1,125 |
| 10,000 | 14,999 | 150 | 320 | 470 | 200 | 320 | 520 | 1,000 | 320 | 1,320 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 610 | 970 | 550 | 610 | 1,160 | 1,450 | 610 | 2,060 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 960 | 1,340 | 600 | 960 | 1,560 | 1,850 | 960 | 2,810 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 1,100 | 1,500 | 680 | 1,100 | 1,780 | 1,850 | 1,100 | 2,950 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 1,500 | 1,910 | 750 | 1,500 | 2,250 | 2,350 | 1,500 | 3,850 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 2,050 | 2,770 | 1,250 | 2,050 | 3,300 | 2,700 | 2,050 | 4,750 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 2,530 | 3,530 | 1,600 | 2,530 | 4,130 | 3,650 | 2,530 | 6,180 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 2,940 | 4,140 | 1,900 | 2,940 | 4,840 | 5,300 | 2,940 | 8,240 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 3,500 | 5,000 | 2,300 | 3,500 | 5,800 | 6,500 | 3,500 | 10,000 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 4,100 | 5,600 | 2,500 | 4,100 | 6,600 | 7,000 | 4,100 | 11,100 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 5,200 | 7,400 | 3,200 | 5,200 | 8,400 | 7,500 | 5,200 | 12,700 |
| 600,000 | 699,999 | 2,200 | 6,400 | 8,600 | 3,200 | 6,400 | 9,600 | 7,500 | 6,400 | 13,900 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 7,100 | 10,400 | 4,300 | 7,100 | 11,400 | 8,000 | 7,100 | 15,100 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 7,520 | 11,020 | 4,300 | 7,520 | 11,820 | 8,000 | 7,520 | 15,520 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 8,900 | 12,400 | 6,000 | 8,900 | 14,900 | 8,000 | 8,900 | 16,900 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 9,400 | 14,400 | 6,000 | 9,400 | 15,400 | 8,000 | 9,400 | 17,400 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 10,000 | 15,000 | 6,000 | 10,000 | 16,000 | 10,000 | 10,000 | 20,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa Pesa kwa mteja ambaye amesajiliwa ila hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika.**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea tovuti; **https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:** LiPa kwa simu

**KUMBUKA:**

1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 5,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 0713800800 au 0713123103 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwa barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Afrika Mashariki.
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#** chagua **6 (Jihudumie)** kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

**App yenye urahisi wa kushangaza!**




**Fanya malipo ya Serikali**

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia July 2021

tigo

www.tigo.co.tz

# Anayedaiwa kuua mwanawe auawa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKAZI wa Kitongoji cha Kaloleni Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Alon Cardius (27), ameuawa kwa kipigo kutoka kwa wananchi wanaodaiwa kuwa wenye hasira kali baada ya kutuhumiwa kumuua mtoto wake kwa kumkata panga.

Tukio la kuuawa kwa mtuhumiwa huyo likitokea Julai 13 majira ya saa tatu asubuhi katika Kijiji cha Isesa alipokuwa amekwenda ukweni kwake ili kudai apewe mke wake baada ya mkewe huyo kuondoka nyumbani kwao kutokana na migogoro ya kifamilia.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, William Mwampaghale, baada ya kutofautiana, mke aliamua kukimbilia nyumbani kwao akihofu usalama wake kwa madai kuwa mume wake ni mkorofi.

Taarifa hiyo ilidai kuwa baada ya mama kukimbilia kwao, alimwacha mtoto wake aitwaye Charles Cardius na baba yake, lakini mume wake huyo anadaiwa kumuua mtoto huyo kama njia ya kushinikiza mke wake arudi nyumbani ili waendelee kuishi pamoja.

"Baada ya kufanya mauaji hayo, Jeshi la Polisi lilianza kumsaka kwa tuhuma za kumuua mtoto wake ndipo alipokimbilia mkoani Mbeya kujificha.

"Baada ya wiki mbili, alirudi Kijiji cha Isesa kwa lengo la kumuua baba mkwe wake, akidai kuwa ndiye anayemzuia binti yake asirudi nyumbani kwake.

"Alipofika katika kijiji hicho alianza kujisifu kuwa amerudi kumuua baba mkwe wake, ndipo wananchi walipokasirika na kumvamia kumpiga hadi kumsababishia kifo chake hapo hapo," taarifa ya Jeshi la Polisi ilibainisha.

Kamanda Mwampaghale aliwaonya wananchi dhidi ya tabia za kujichukukia sheria mikononi, badala yake wawe wanawakamata watuhumiwa na kuwafikisha mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

# Watatu walazwa Z'bar kwa corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HOSPITALI ya Rufani ya Mnazimmoja Zanzibar imepokea wagonjwa watatu wa corona ambao wanaendelea kupatiwa matibabu.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Hospitali hiyo, Dk. Abdulrahman Khalfan Said. Alisema kutokana na uwapo wa ugonjwa huo Zanzibar ni marufuku kwa mtu yeyote kuingia hospitalini hapo bila ya kuvaa barakoa.

Alisema hospitali ni sehemu hatarishi, hivyo wananchi wanapaswa kuvaa barakoa muda wote kama njia ya tahadhari.

Mkurugenzi huyo alieleza kuwa wana upungufu wa barakoa hospitalini hapo na ndio maana wanatoa barakoa kwa wahudumu wa afya pekee, lakini kwa wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wanatakiwa kujigharamia wenyewe kuzinunua.

"Tunatamani watu wote wanaofika hapa kuwapatia barakoa, lakini tunashindwa, kutokana na uhaba tulionao, ndio maana tumeshatoa tangazo kwa wananchi kuwa wanapofika hospitalini hapa kufuata huduma au kuwaangalia ndugu zao waliolazwa kuja na barakoa," alisema.

Akizungumzia kuhusu gesi ya Oksijeni hospitalini hapo, alisema kwa siku wanatumia mitungi 45 kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wengine. Aidha, mkurugenzi huyo aliwataka wafanya biashara na watu wenye uwezo kuanzisha viwanda vya upatikanaji wa oksijeni Zanzibar kwa sababu huduma hiyo wanaagiza kutoka Tanzania Bara.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga wa hospitali hiyo, Haji Nyonge Pandu, alisema hospitali hiyo inapokea wastani wa wagonjwa 300 kwa siku na kuthibitisha kuwapo kwa baadhi ya huduma zisizoridhisha kutokana na upungufu wa vitendea kazi.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akizungumza kwenye kongamano la maofisa watendaji wakuu wa taasisi mbalimbali za sekta binafsi (CEOrt), jijini Dar es Salaam jana, lenye lengo la kuona jinsi gani sekta binafsi zitashirikiana na mipango ya serikali ya maendeleo ya miaka mitano ijayo ya kukuza uchumi wa Taifa. Kulia ni Mwenyekiti wa CEOrt, Sanjay Rughani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wastaafu watahadharishwa mikopo umiza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANACHAMA wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) wanaotarajia kustaafu, wametakiwa kujiepusha kutumia mafao yao kufanya biashara na taasisi za fedha zisizoeleweka.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alitoa tahadhari hiyo jana alipokuwa akifungua semina ya wastaafu watarajiwa wa PSSSF kwa mwaka wa fedha 2021/22 na mwaka 2022/23 jijini hapa.

Mtaka alisema kwa sasa kuna wimbi la kesi nyingi za wastaafu kutapeliwa mafao yao ambazo nyingi zimekuwa zikiwasilishwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Alisema muda wa kustaafu ukifika kunakuwa na washauri wengi kutoka kila kona, ikiwamo utapeli wa biashara za mitandaoni jambo ambalo wengi huzifuata na kuamini kuwekeza fedha mwisho wa siku wanakuja kutapeliwa.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wastaafu hao kuwa makini na mafao yao na kutokubali kurubuniwa na watu wanaojifanya wanakopesha fedha au wajenzi wa nyumba za bei nafuu.

"Ninawaomba kuweni makini na hiyo ni fedha yako usikubali kubabaishwa. Nawaomba wastaafu watarajiwa kuweni makini sana na fedha zenu. Tulieni mfanyie kitu cha maana na si kufanya biashara na watu usiowajua, baadaye uanze kuzunguka katika taasisi kuomba msaada wa kupata haki yako," alisema Mtaka.

Aliwataka wastaafu watarajiwa kama wamekopa fedha za riba kwa watu binafsi au taasisi binafsi wakatoe taarifa katika ofisini yake ili kusaidiwa namna ya kufanya.

Alisema taasisi binafsi zimekuwa zikiwasiliana na maofisa utumishi ili kujua mafao ya mhusika yanaingia lini waende kuchukua fedha za mkopo ambazo mhusika alikopa.

"Wastaafu wanapaswa kulijua hilo hivyo mkiwa mmebakiza muda mchache wa kustaafu fanyeni masuala yenu kwa umakini na watu makini kama benki," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Mbaruku Magawa, alisema wastaafu ni miongoni mwa walengwa na waathirika wa utapeli, uhalifu na rushwa.

"Kutokana na ongezeko la utapeli, uhalifu wa kimtandao na rushwa ambapo wastaafu ni miongoni mwa walengwa na waashirika wa uhalifu huo, hivyo katika mafunzo haya yatajumuisha wataalamu kutoka TAKUKURU na TCRA ili kuwajengea uwezo wa kubaini na kuchukua tahadhari juu ya uhalifu huo," alisema Magawa.

Alisema mafunzo hayo hufanyika kila mwaka kwa wanachama waliobakiza kipindi kisichozidi miaka miwili kabla ya kustaafu yanafanyika nchi nzima.

Magawa alisema mafunzo hayo yameshirikisha taasisi saba za fedha ili kuwapa elimu juu ya uwekezaji na matumizi sahihi ya fedha.

# Taasisi za fedha zapewa elimu mpya

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

TAASISI za fedha nchini zimetakiwa kutoa elimu na ushauri wa miradi kabla ya kutoa mikopo kwa wahusika ili kuondokana na wimbi la watu kushindwa kurejesha na kufilisiwa mali zao.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipokuwa akizindua taasisi ya kutoa mikopo ya K-Finance Tawi la Dodoma.

"Kuna baadhi ya taasisi za kifedha zimekuwa na tabia ya kuwashawishi wananchi kuchukua mikopo badala ya kutoa elimu kabla ya kutoa," alisema.

Shekimweri alisema wakati wa kuwashawishi wananchi kuchukua mikopo, wanakuwa na lugha laini lakini wakati wa kuwadai wanakuwa wakali na kuwanyang'anya mali zao.

Pia alizitaka taasisi hizo kuhakikisha wanawafikia wakulima kwa kuwa mikopo hiyo itasaidia kuinua uchumi wa wakulima, hivyo kuwahimiza wananchi wanaochukua mikopo kwenye taasisi hizo kujenga tabia ya uaminifu na kurejesha kwa wakati.

Mwenyekiti wa Bodi ya K-Finance, Devotha Minzi, alisema kampuni hiyo ilisajiliwa na kuanza kutoa huduma zake mwaka 2008 mkoani Dar es Salaam na imekuwa ikitoa huduma za mikopo ya kifedha kwa wananchi wa kawaida na wafanyakazi wa serikali na kampuni binafsi.

Mkurugenzi Mtendaji wa K-Finance, Judith Minzi, alisema wamepokea leseni kama taasisi ya kifedha chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) hivi karibuni na wanatoa mikopo kuanzia kiasi kidogo hadi kiwango cha juu cha Sh. milioni 50 kwa mtu binafsi au kampuni.

Alisema wanatoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo kwa asilimia tatu hadi tano na mkopo kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo kwa riba nafuu ambazo zitawafanya waendeleza biashara na miradi yao.

Aliongeza taasisi hiyo inatoa mikopo ya afya ambayo itamwezesha mkopoji kuchukua muda mfupi ili kufanikisha matibabu na pia mikopo kwa ajili ya elimu ambayo itamsaidia mhusika kulipa ada ya masomo.

# Msajili, CHADEMA watunishiana misuli

**Na Enock Charles**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imekiandikia barua Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kukitaka kieleze sababu za kuwafuta uanachama wabunge 19 watokanao na chama hicho.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kigaila, alibainisha chama hicho kupokea barua kutoka Ofisi ya Msajili, alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana.

Novemba 27, mwaka jana, Kamati Kuu ya CHADEMA ilitangaza kuwafukuza uanachama wabunge 19 wa viti maalum, wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee.

Kigaila alisema jana kuwa wakati rufani ya wabunge hao ikisubiri kujadiliwa na Baraza Kuu la CHADEMA, chama hicho kilipokea barua kutoka kwa Msajili Julai 6, mwaka huu, akikitaka kuwasilisha kwake maelezo kuhusu kufukuzwa uanachama kwa wabunge hao.

"Msajili katika barua yake (akiionyesha kwa waandishi wa habari) anasema kuna watu wamewasilisha malalamiko kwake wakimlalamikia kwamba hawakubaliani na tamko la chama la kuwafukuza uanachama.

"Yeye ni mwanasheria, anajua kwamba huwezi kuwasilisha maelezo kuhusu malalamiko ambayo hujayapata. Yeye amesema amepokea malalamiko lakini hajaambatanisha barua za malalamiko ya hao watu.

"Tumemjibu na Watanzania waelewe na yeye atuelewe. Kuna upungufu wa aina mbili. Kwanza; kutaka tutoea maelezo bila kutupatia malalamiko.

"Pili; Msajili kuingia ndani ya suala ambalo halijakamilishwa ndani ya chama huku akijua hao walalamikaji wamekata rufani. Alipaswa kuwaambia kwamba 'ninyi mmekata rufani, subirini uamuzi wa Baraza Kuu," alisema.

Kigaila alisema kitendo cha Msajili kuwaandikia barua wanakiona kama ni njama za kulizuia Baraza Kuu la CHADEMA kufanya kazi yake ya kujadili rufani na kutoa uamuzi kwa mujibu wa katiba.

"Tunatoa maelezo kwake kama nani? Kama chombo gani? CHADEMA ina katiba, ina vyombo vyake, na vyombo vyake ndivyo vitakavyotumika.

"Kama kuna maelezo kwa nini walifukuzwa, yatapelekwa Baraza Kuu na siyo kwa Msajili kwa sababu Msajili siyo chombo cha rufani na wala siyo mahakama.

"Tumemwandikia barua tarehe 9 (Julai 9) na aliweka siku ya mwisho ya barua (ya majibu) kumfikia tarehe 10 (Julai 10) na sisi tuliifikisha kwake ofisini Dodoma tarehe 10," alisema.

Alidai kuwa Msajili amejiingiza kwenye jambo ambalo halimhusu.

Kwa takriban miezi sita sasa, kumekuwa na mvutano kati uongozi wa CHADEMA na Bunge la Tanzania kuhusu uhalali wa wabunge 19 wa viti maalum wanaotokana na chama hicho.

Baada ya kuapishwa na Spika Ndugai kuwa wabunge wa Bunge la 12, chama hicho kupitia kwa Katibu Mkuu wake, John Mnyika, kilidai hakitambui nyaraka zote zilizowasilishwa bungeni kuhalilisha uteuzi wa wabunge hao.

Mbali na Mdee, wabunge wengine wanaohusika na sakata hilo ni pamoja na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA, Hawa Mwaifunga, Katibu Mkuu Grace Tendega, Naibu Katibu Mkuu Bara, Jesca Kishoa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Asia Mohamed, Katibu Mwenezi Agnesta Lambert, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana Nusrat Hanje na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti Ester Matiko.

Wengine ni Cecilia Pareso, Tunza Malapa, Ester Bulaya, Felister Njau, Sophia Mwakagenda, Ngahenjwa Kaboyoka, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Conchesta Rwamlaza, Salome Makamba na Stella Fiao.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kushoto), akiwasikiliza wananchi waliotembelea kwenye banda la mfuko huo ili kupata elimu ya fidia wakati wa Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofikia kilele juzi. Mfuko huo umeibuka mshindi katika kundi la Taasisi za Bima na Hifadhi ya Jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau usafirishaji waonywa kuhusu corona

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, amewataka wasafirishaji na wasafiri kuzingatia uvaaji barakoa na kukaa kwa umbali kwenye vyombo vya usafiri ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kuzindua Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), jijini Dar es Salaam juzi, alisema Wizara imetoa mwongozi unaopaswa kuzingatiwa kwa wasafirishaji na wasafiri wote wa majini na nchi kavu.

"Tunatoa rai watu wote wavae barakoa na kuachiana nafasi ili tujitahidi kuwa salama katika mlipuko huo. Uvaaji barakoa ni muhimu sana ili tuwe salama," alisema.

Chamuriho alisema: "Nimetoa mwongozo kwa wasafiri wote wa njia ya barabara, anga na njia nyingine, hii ni kulingana na maelekezo tuliyopewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Ninatoa rai kwamba wote tuwe waelewa kwamba ugonjwa huu tunao, upo. Rais Samia Suluhu Hassan ametoa hadi takwimu kwamba upo ni jukumu letu kusikiliza tunayoelekezwa kwamba tuchukue tahadhari."

Aidha, alisema wizara hiyo inazingatia kikamilifu mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya na ni lazima ufuate, na kwamba kuchukua hatau dhidi ya wanaokaidi bado haijafika huko, lakini ikifika wakati wizara hiyo ikaagiza watafanya hivyo.

Juni, mwaka huu, Rais Samia alitangaza kuwapo kwa ugonjwa wa UVIKO awamu ya tatu, na mara kadhaa amekuwa akiwataka Watanzania kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kuepuka misongamano na kunawa mikono na maji tiririka na sabuni.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Alama ya Mkapa madarakani iwafundishe viongozi wengine

**JANA** ilikuwa ni kumbukizi ya mwaka mmoja tangu kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin Mkapa, aliyezaliwa katika Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi, mkoani Mtwara, kukiwa na mjadala na salamu kutoka kwa watu maarufu duniani, katika kongamano hilo ambalo mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Hayati Mkapa ni rais ambaye atakumbukwa kwa mengi ambayo alijenga msingi thabiti na hadi sasa yanaendelea na yataendelea kugusa maisha ya kila Mtanzania, pia viongozi wa kimataifa wamepaza sauti kupitia mtandao na wengine walikuja nchini kwa ajili hiyo, akiwamo Rais mstaafu wa Marekani, Bill Clinton na Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair.

Alama za Hayati Mkapa zinaishi na zimeendelea kuisaidia nchi hasa katika uanzishaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), akiwa na kaulimbiu ya kodi kwanza, pia alianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ambao umeendelea kuwapo hadi sasa.

Alama nyingine ni kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mfuko wa Barabara ambao uliwezesha kujengwa kwa barabara nyingi za kuunganisha mikoa, wilaya na kazi ambayo iliendelezwa na Rais wa Awamu ya nne, Jakaya Kikwete na baadaye Hayati Joseph Magufuli.

Aidha, Mkapa ameacha alama ya kupambana na umaskini kwa kuanzisha Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), pia wakati wake ulianzishwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), ambao ulilenga kuinua hali ya maisha ya mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Kwenye elimu Mkapa anakumbukwa kwa kuanzisha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) na Mpango wa Elimu ya Sekondari kwa Walioikosa (MMES) na shule za mwanzo kabisa za kata ambazo zilisaidia wanafunzi wengi kuendelea na masomo ya sekondari, kutokana na wengi kufaulu, lakini wapo waliokaa nyumbani kwa kukosa shule za kwenda kusoma na kuanzia hapo rais aliyefuata aliendeleza utaratibu huo na kukawa na mwamko mkubwa wa kila kata kuwa na shule ya sekondari.

Kutokana na mipango hiyo watu wengi walijiendeleza kielimu na kuwa na elimu ya msingi, sekondari na baadhi walifika hadi vyuo vikuu, walimu wa UPE (Universal Primary Education) walijiendeleza na kupata vyeti vya kidato cha nne na sita, huku wengine wakifika vyuo vikuu na hata walivyostaafu walikuwa kwenye hali nzuri zaidi ya kipato kutokana na kupanda madaraja.

Eneo jingine ni kwenye afya ambalo baada ya kustaafu alianzisha Mkapa Foundation ambayo ilijikita kwenye kuboresha afya maeneo ya vijijini ikiwamo kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali na kuikabidhi serikali, pamoja na kutoa vifaa tiba muhimu.

Hali hii ilisaidia sana maboresho makubwa ya huduma za afya hasa vijijini na hadi sasa wameendelea na kazi hiyo, na pia anakumbukwa kwa kuanzisha Tume ya Ukimwi Tanzania (TACAIDS), ambayo ilisaidia mengi kwenye eneo hilo ikiwamo kutoa afua mbalimbali, elimu ya Ukimwi na udhibiti ikiwamo kuwa na miongozo mbalimbali ya utaoji huduma.

Pia Mkapa alianzia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ambayo imesaidia kupambana na rushwa na kuna nyakati ilionekana kushamiri kiasi cha huduma muhimu za kijamii kuuzwa badala ya kutolewa bure.

Alama ya Mkapa ipo pia kimataifa kiasi cha kushirikishwa kwenye utatuzi wa migogoro mingi na unaokumbukwa sana ni wa mwaka 2007 nchini Kenya, baada ya uchaguzi Mkuu ambao ulitawaliwa na vurugu na vifo vya baadhi ya watu, lakini kwa kushirikiana na viongozi wengine Mkapa aliongoza timu ya usuluhishi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

### Lawama imekaa upande gani, Zimamoto na janga Kariakoo?

**JESHI** la Zimamoto na Uokoaji limekuwa likilalamikiwa na jamii kwa mambo mawili, mojawapo ni kwa kuchelewa kufika kwenye matukio na pia kutokuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya kuzima moto.

Lawama hizo huwa zinasukumwa kwenye jeshi hilo, kutokana na kwamba, wakati mwingine sababu hizo ndizo zinazochangia baadhi ya majengo kuteketea bila askari wake kufika kwa wakati au wakiwa hawana maji.

Ni katika mazingira hayo, askari wa jeshi hilo waliwahi kuripotiwa na vyombo vya habari kwamba walinusurika kupigwa na wananchi wenye hasira mjini Shinyanga, baada ya kuchelewa kufika kwenye tukio la nyumba iliokuwa ikiungua moto huku watoto wakiwa ndani.

Yawezekana kuchelewa kufika kwenye matukio ya kuzima moto kukawa na sababu za msingi kama vile miundombinu ya barabara ambayo huchangia magari kukosa sehemu ya kupita.

Kwa mfano katika jiji la Dar es Salaam, barabara zake huwa zimejaa magari, lakini wakati mwingine maeneo ambayo kuna tukio la nyumba kuwaka moto halina barabara ya kupitisha magari.

Zipo sababu nyingine za kuchelewa kufika katika tukio, zinazoelezwa Kamishna Jenerali wa jeshi hilo, John Masunga kwamba, ni kutopewa taarifa mapema kwa kuwa wananchi huanza kushughulikia tatizo wenyewe kabla ya kushindwa na kisha ndipo hupiga simu.

Katika mazingira ya aina hiyo, wakati mwingine inaweza kuwawia vigumu askari wa kikosi hicho kufika kwa wakati ili kutoa huduma na hivyo, kujikuta wakilaumiwa kwa sababu ambazo ziko juu ya uwezo wao.

Lakini pamoja na hayo, ni vyema jeshi hilo likawa na maji ya kutosha kwa ajili kuzimia moto. Ninadhani hilo liko ndani ya uwezo wao, kwa maana kwamba wanatakiwa kuhakikisha yanakuwapo muda wote.

Wiki iliyopita, Soko Kuu la Kariakoo, lililopo jijini Dar es Salaam, liliungua kwa moto, uliozuka kuanzia wastani wa saa 3.00 usiku, lakini kama ilivyozoeleka, lawama zilielekezwa kwa jeshi hilo.

Jeshi hilo lililalamikiwa kwa madai ya kutokuwapo maji ya kutosha kuzima moto huo kwa haraka, hali ambayo kama ina ukweli ndani yake, basi ingefaa kurekebishwa ili kuondokana na lawama za kila mara.

Hata hivyo, niliusikia uongozi ukitamka kuwa, tayari ukifafanua walakini katika vigezo vingine na si shida ya maji.

Pia Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, ameshatoa sababu ya kuchukua muda mrefu kudhibiti moto huo kuwa ni namna ya kutokuwa na sehemu sahihi za kuchukua maji ndani ya Kariakoo.

Ni hali iliyolazimisha wafuate eneo la Ukonga, palipo Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, wastani wa kilomita 10 kutoka penye tukio, huku moto ukiendelea kuteketeza mali za wafanyabiashara ndani ya maduka sokoni.

Daima, binadamu huwa wanajifunza kutokana na makosa, hivyo si vibaya makosa hayo ya kukosa maji jirani na Kariakoo, ikageuka kuwa funzo linalolenga mabadiliko chanya, kwa kutenga sehemu ya maji karibu na maeneo yote.

Hebu tufikirie jambo hilo kwa kina, kwamba kutoka makao makuu ya jeshi hilo, Upanga hadi sokoni Kariakoo si mbali sana, wastani wa chini ya kilomita moja, askari wa Zimamoto na Ukoaji wanaenda mbali zaidi ya kilomita 10 kufuata maji ya kuzimia moto.

Jeshi hilo lina jukumu la kutoa huduma kwa jamii katika nyanja mbalimbali, zikiwamo kuokoa maisha ya watu na mali zao, kuzima moto, kutoa elimu ya kinga na tahadhari ya majanga moto.

Vilevile, Zimamoto na Uokoaji, hufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto, kusoma ramani za majengo na kutoa ushauri, huduma ya kwanza katika majanga na ajali barabarani, kutoa mafunzo ya kukabiliana na majanga moto, uchunguzi katika majanga ya moto na huduma za kibinadamu.

Hivyo, zinapojitokeza kasoro kama za Kariakoo, ziwe fursa ya kufanya marekebisho, ili kuondoa lawama zisizo za lazima kutoka kwa watu, ambazo baadhi yao wanaamini kwamba jeshi hilo halifanyi kazi yake kikamilifu.

Inavyofahamika, magari ya zimamoto yanapofika kwenye tukio, hufanya kazi kama mtambo wa kuzimamoto kutokanana jinsio yalivyotengezwa yakiwa na matangi ya maji yenye ujazo kuanzia lita 1,500 hadi lita 7,000.

Ilivyo, katika ufafanuzi huo wa kitaalamu, ili maji hayo yatoke kwa nguvu na kuweza kuzima moto, kwa kawaida magari ya jeshi hilo huwa yamefungwa pampu zenye uwezo wa kusukuma lita 2,000 hadi lita 6,000 kwa dakika.

Hayo yakifanyika kama inavyotakiwa, hakutakuwapo lawama kwa jeshi hilo, lakini kwenye suala la kuchelewa kufika kwa wakati mwingine, inaweza kuwa nje ya uwezo wa jeshi husika.

# Kizimbani tuhuma ya kubaka mtoto

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MKAZI wa Kijiji cha Ibutamisuzi, Kata ya Mbutu wilayani Igunga mkoani Tabora, Yohana Jibamabi (47), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Wilaya ya Igunga kwa tuhuma ya kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 13.

Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Igunga, Elimajid Kweyamba, alidai mahakamani huko kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 130(1) cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 na mapitio yake ya mwaka 2019.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Lyidia Ilunda, Kweyamba alidai kuwa Aprili 3, mwaka huu, majira ya saa nne usiku, katika Kijiji cha Ibutamisuzi, Kata ya Mbutu, mshtakiwa huyo alimbaka mtoto huyo (jina limehifadhiwa).

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka dhidi yake, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo na kesi imeahirishwa hadi Julai 23 mwaka huu itakapoanza kusikilizwa na mshtakiwa yupo nje kwa dhamana baada ya kukidhi masharti ya kuweka bondi ya Sh. milioni tatu.

# Watoto waliozaliwa njiti wawezeshwa

**Na Christina Mwakangale**

MIKOA minane imenufaika na msaada wa kupatiwa vifaa vya afya ikiwamo maalumu kwa ajili ya kupunguza vifo vya watoto njiti vitokanavyo na matatizo mbalimbali.

Kampuni ya simu ya Vodacom Tanzania Plc kupitia Taasisi ya Vodacom Foundation kwa kushirikiana na Taasisi ya Doris Mollel Foundation (DMF), wametoa vifaa hivyo kwenye mikoa hiyo ukiwamo Kigoma.

Mikoa mingine iliyonufaika kwa kupatiwa vifaa hivyo ikiwamo oksijeni ni Tabora, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Lindi na Pwani.

Msaada uliotolewa mwaka jana ulikifikia kituo cha afya kilichopo jijini Arusha, uliogharimu Sh. milioni 32 huku Hospitali ya Kibaha, ikipokea vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 58 na kituo cha afya Mlele, Kibaha kikipata vifaa vya Sh. milioni 50.

Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, alisema vifaa vilivyotolewa ni mablanketi, vifaa vya kulishia chakula na oksijeni kwa ajili ya watoto njiti, ambao kwa kiasi kikubwa huhitaji joto.

"Taasisi imesaidia kujenga kujenga miundombinu ya afya baada ya kumaliza awamu ya kwanza, kitu cha Moyo Center kilichopo Hospitali ya CCBRT, itakuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wanawake 12,000 kwa wakati mmoja.

"Tunafarijika kusaidia na kuboresha huduma za afya ya kinamama nchini kwa sababu ni eneo ambalo tunaona ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu. Kwa zaidi ya miaka 10, msukumo wa kuboresha afya ya Watanzania kwa kutumia teknolojia ya mtandao wetu."

"Michango hii haijaishia tu katika mikoa iliyotajwa hapo juu bali imesambaa nchini kote na kutambulika kuwa na mafanikio makubwa. Hivi karibuni, asasi ya Vodacom Tanzania Foundation ilitambuliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano wake na Jumuiya ya Msalaba Mwekundu."



Meneja wa maduka ya rejareja ya Vodacom Tanzania Plc, Vanessa Mlawi akionyesha tuzo baada ya kuibuka kinara katika utoaji wa huduma bora katika sekta ya mawasiliano kwenye maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri asikiliza kero 120 za ardhi Morogoro

**Na Munir Shemweta,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesikiliza kero 120 za ardhi ndani ya siku mbili na kuzipatia ufumbuzi baadhi ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Mabula ambaye alianza kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero za ardhi juzi katika wilaya ya Kilosa na jana alikutana na wananchi wenye kero hizo kwenye mkutano wa hadhara eneo la stendi ya Mafiga Manispaa ya Morogoro.

Akiwa ameambatana na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, Katibu Tawala Mariam Mtunguja na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Morogoro Frank Minzikuntwe, na wataalamu wa Sekta ya Ardhi kutoka Manispaa ya Morogoro, Mabula alimpa fursa kila mwananchi mwenye kero ya ardhi aliyefika kuwasilisha kwa uwazi na kuwataka wahusika kujibu hoja kabla ya kutoa uamuzi.

Kero nyingi za ardhi zilizowasilishwa katika Manispaa ya Morogoro ni juu ya wananchi kudhulumiwa maeneo, umilikishaji ardhi mara mbili na madai ya fidia kutokana na kuchukuliwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Akizungumnza wakati wa kuzipatia ufumbuzi kero ambazo baadhi ni za miaka ya 1990. Dk. Mabula aliwataka wananchi kuwa makini wakati wa kuuziwa maeneo na kuhakikisha wanapotaka kununua ardhi waulizie ofisi za ardhi ili kujua wamiliki pamoja na matumizi ya eneo husika.

"Mnapotaka kununua eneo lazima mkaulizie ofisi za ardhi ili kujua kama eneo hilo limemilikishwa kwa mtu mwingine au matumizi ya eneo hilo ni yapi maana unaweza kuuziwa eneo kumbe ni la wazi," alisema.

Dk. Mabula aliwaagiza watendaji wa sekta ya ardhi kudhibiti ujenzi holela sambamba na kuhakikisha hakuna mtu anayejenga bila kuwa na kibali na ujenzi wowote unaofanyika unazingatia mipango miji ya eneo husika.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Msando, alimpongeza Naibu Waziri kwa kusikiliza kero 120 za ardhi katika wilaya mbili za Kilosa na Morogoro na kusema hatua hiyo inafanya wilaya yake kuongeza juhudu za kushughulikia kero za ardhi tofauti na malengo ya kusikiliza kero mia tano kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Msando, Wilaya ya Morogoro imejiwekea malengo ya kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero mia tano za ardhi katika kipindi cha mwaka mmoja.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Minzikuntwe alisema katika mkutano huo kuwa migogoro mingi ya ardhi kwenye mkoa imesababishwa na ununuzi holela wa ardhi unaofanywa na wananchi hasa kupitia watendaji mitaa au wenyeviti wa vijiji.

"Migogoro mingi hapa morogoro imesababishwa na wananchi kununua ardhi kiholela bila kupitia ofisi za ardhi ambazo ndizo zenye kumbukumbu za wamiliki," alisema.

Naibu Waziri Mabula alimaliza ziara yake jana mkoani Morogoro na anaendelea katika mkoa wa Dodoma eneo la Kibaigwa ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia aliyemtaka kwenda kusikiliza na kuzipatia ufumbuzi kero za ardhi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa maeneo hayo.

# Machinjio yamshtua waziri

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Hamad Chande, amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Tina Sekambo, kuhakikisha anafanya ukarabati haraka wa mfumo wa majitaka katika machinjio ya Songea ili kulinda mazingira.

Chande alitoa maagizo hayo juzi baada ya kufanya ziara ya kikazi kukagua uzingatia na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika Mkoa wa Ruvuma.

Akiwa katika machinjio hayo, Naibu Waziri Chande alibainisha kusikitishwa na namna machinjio yanavyoendeshwa, akishuhudia usafi wa mazingira usioridhisha ikiwa ni pamoja na utiritishaji wa majitaka katika mtaro usio rasmi, kutapakaa kwa damu katika sakafu na kushuhudia watumishi wakifanya kazi bila vifaa vya usalama mahali pa kazi.

Chande alitoa muda wa siku saba kuanzia jana kwa uongozi wa machinjio hayo kurekebisha dosari zilizojitokeza na kumwagiza Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo na kutoa mrejesho mapema.

Awali, Naibu Waziri Chande alitembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea na kutoa rai kwa uongozi wa wilaya kusikiliza na kupatia ufumbuzi kero za wakazi wanaozunguka maeneo hayo ili wawe walinzi wa mazingira na miundombinu inayozunguka vyanzo hivyo.

"Ndugu zangu, maji ni uhai, ninatoa rai kwenu kulinda vyanzo vya maji katika milima hii ya Matogolo kwa kudhibiti shughuli za kibinadamu zisizo endelevu," Chande alisisitiza.

Akitoa taarifa ya hali ya mazingira katika mkoa wake, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Willbert Ibuge, alisema mkoa unakabiliwa vikwazo vya kilimo cha kuhamahama, uchomaji holela wa mkaa, uvamizi na uchomaji holela wa misitu.

Alisema jitihada zimefanyika kwa kushirikiana na wadau wa maziringa ili kukabiliana na vikwazo hivyo ikiwa ni pamoja na kuwaondoa wavamizi wote waliopo kwenye hifadhi za misitu zikiwamo za Bonde la Rufiji.

Naibu Waziri Chande yuko mkoani Ruvuma katika ziara ya kikazi kukagua utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Katika siku ya kwanza ya ziara yake juzi, alizuru Manispaa ya Songea na jana alikuwa wilayani Mbinga.

Mgodi wapewa siku 14 kudhibiti maji taka.

Serikali imesema uwekezaji wowote ni lazima uzingatie Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake ikiwa ni pamoja kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kuwa ni takwa la kisheria.

Hayo yamesemwa leo wilayani Mbinga na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Hamad Hassan Chande baada ya kufanya ziara ya kukagua migodi ya uchimbaji wa makaa ya mawe ya Tancoal Ltd na Ruvuma coal.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri Chande ametoa siku 14 kwa Mgodi wa Tancoal kudhibiti majitaka katika mabwawa yao pamoja na kudhibiti vumbi ambalo limekuwa kero kwa wakazi wa maeneo ya jirani.

"Mazingira ndio uhai wetu, tuyatunze na tuyalinde kwa gharama yoyote ile," Chande alisisitiza.

Chande ameshuhudia ukataji wa miti kwa kiwango kikubwa katika migodi hiyo na kuagiza migodi yote miwili kuandaa mpango wa muda mfupi wa upandaji miti ili kurejesha uoto wa asili.

# Utafiti wa mahitaji viwanda waagizwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, ameviagiza vyuo vikuu nchini kufanya utafiti wa mahitaji halisi kwenye viwanda ili vitumike kukuza uchumi.

Alisema kufanya tathmini kwenye viwanda hivyo kutasaidia pia kufahamu mahitaji halisi ya rasilimali watu na pia itasaidia kupunguza tatizo la ajira.

Pia, ameziagiza taasisi zinazosimamia wafanyabiashara na wazalishaji kutoka pande zote za Muungano kutatua changamoto ambazo bado zinaonekana ni kikwazo kwa biashara.

Abudullah alitoa agizo hilo juzi jioni wakati akifunga Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Saalam aliyoanza Juni 28, mwaka huu. Alisema kutatua changamoto hizo kutasaidia wafanyabiashara na wazalishaji kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Pia aliagiza kuhakikisha kwamba bidhaa za ndani na vifungashio vinaboreshwa zaidi kukidhi soko la kimataifa. Alitoa wito kwa wazalishaji wa Tanzania kupeleka bidhaa zao nje ya nchi.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar, Omary Said Shaaban, alisema maonyesho ya mwaka huu yameakisi lengo la kuyafanya kuwa ya kimataifa.

Alisema maonyesho hayo yamekuwa sehemu kubwa ya kujitangaza na kubadilishana uzoefu katika maeneo yao ya kufanyia kazi.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mpaka juzi asubuhi watu waliokuwa wametembelea maonyesho hayo mwaka huu walikuwa 227,000.

Alisema bidhaa zilizoongoza kuuzwa ni za kitanzania, ambazo ni mazao ya kilimo, korosho, chai na kahawa.

Pia alisema katika maonyesho hayo, bidhaa za ngozi nazo zimeuzwa kwa kiwango kikubwa. Alisema mwakani wamepanga maonyesho hayo yawe makubwa zaidi.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (katikati), akifurahia pamoja na baadhi ya wafanyakazi wenzake, baada ya kutangazwa mshindi wa tatu mwonyeshaji bora katika sekta ya watoa huduma za afya, katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika, katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Malaria yatajwa tishio kubwa Afrika

**NA Frank Kaundula,** MOROGORO

SHIRIKA lisilo kiserikali la India AJANTA FARMER limetoa elimu ya kupambana na ugonjwa wa malaria kwa madaktari bingwa mkoani Morogoro ili kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa huo hasa barani Afrika.

Akizungumza na madaktari hao, Mkurugenzi wa shirika hilo upande wa Tanzania, Kumar Bangali, alisema hatua hiyo imechukuliwa baada ya utafiti mbalimbali uliofanyika kuonyesha Bara la Afrika ndio linaongoza kwa vifo vitokanavyo na malaria kwa zaidi ya asilimia 90.

Alisema miongoni wa sababu zinazosababisha ugonjwa huo kuendelea kuchukua maisha ya watu wengi ni matumizi yasiyosahihi ya dawa na kushindwa kumaliza dozi kama inavyoshauriwa na wataalamu, kwa kisingizio cha wingi wa dawa ambazo huchukua muda mrefu kuisha.

"Takwimu zinaonyesha Afrika ndio bara linaloongoza kwa vifo kwa asilimia 90 ndio maana shirika letu limejikita katika kutafuta suluhu ya changamoto hii kwa kuwashirikisha madaktari bingwa na kuwapa elimu, kwa kusisitiza matumizi sahihi ya dozi ambayo haitamchosha mgonjwa," alisema Bangali.

Abby Kosana, mtaalamu wa dawa katika shirika hilo, alisema ili kukabiliana na changamoto ya kutomaliza dozi kwa baadhi ya wagonjwa, wataalamu wamefanikiwa kutengeneza dozi fupi ambayo haitamchosha mgonjwa.

Alisema dawa ambazo zipo katika dozi mpya zina vidonge sita ambapo mgonjwa akitumia zitasaidia kumalizi kabisa ugonjwa tofauti na awali, ambapo wagonjwa walikuwa wakikatisha dozi wakidhani wamepona.

Aidha, Dk. Kapilia wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), alisema mpango wa kupunguza wingi wa dawa katika dozi ya malaria ni miongoni wa njia sahihi za kukabiliana na changamoto hiyo.

Alisema pamoja na kupunguzwa kwa dozi ni muhimu kuzingatiwa kwa utoaji wa elimu ya matumizi sahihi ya dozi hizo kwa wagonjwa sambamba na kuwapunguzia gharama ili huduma hiyo iwafikie hata kwa wananchi wa kipato cha chini.

HABARI KITAIFA

# Bil. 1.2/- kuendeleza viwanda Bagamoyo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Joydons T. Limited inayojihusisha na uchakataji wa mazao ya mahindi iliyopo Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani imepata mkopo wa Sh. bilioni 1.2 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Mapinduzi ya Kijani Africa (AGRA), kwa lengo la kuongezea uwezo wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya mahindi.

Akizungumza baada ya ziara ya Mwenyekiti wa Bodi ya AGRA, Hailemariam Dessalegn ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Ethiopia aliyeambatana na Rais mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete ambaye ni mjumbe wa bodi hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TADB, Derick Rugemala, alisema ushirikiano huo umetokana na uhitaji mkubwa uliopo kwa wadau wa kilimo.

"Kumekuwa na upotevu mkubwa wa mazao kutokana na kukosa viwanda vya kuchaka mazao hayo, hivyo tumeingia ubia na kampuni hii inayomilikiwa na wanawake ili iweze kusaidia kuondoa upotevu wa mazao kwa kufanya uwekezaji wa kiwanda hapa Bagamoyo," alisema Rugemala.

Alieleza kuwa ukimsaidia mwanamke ni kwamba umeisaidia jamii nzima, hivyo TADB kwa kushirikana na AGRA imeiwezesha kampuni ya Joydons ili kuifikia jamii kwa upana wake kwa kuhakikisha mazao ya mahindi yanakuwa na soko la uhakika.

"Tuna imani kuwa uwapo wa kiwanda hiki hapa Bagamoyo kutasaidia wakulima wa mikoa jirani kuwa na soko la uhakika la mazao yao na kupelekea uchumi katika maeneo haya kuongezeka," alisema Rugemala.

Alieleza kuwa TADB inaendelea kupokea maombi ya mikopo kutoka kwa wadau kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kufanya uzalishaji wenye tija ambao utaifanya nchi kujitosheleza kwa chakula na kuuza nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Bodi ya AGRA, Hailemariam Dessalegn, alisema amevutiwa na uwekezaji uliofanywa na kiwanda cha Joydons, na kwamba kitasaidia katika kuhamasisha kilimo bora kwa ukanda huu.

"Tanzania inaweza kulisha nchi za Afrika endapo mapinduzi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi yakifanyika kikamilifu," alisema Dessalegn na kukitaja kiwanda cha Joydons kuwa kielelezo cha mapinduzi hayo katika kuongezea thamani mazao ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Joydons Tanzania Ltd, Joyce Donati Kimaro, alizishukuru TADB na AGRA kwa kuweza kufanya uwekezaji wa kiwanda hicho na kueleza matarajio yake katika kuwafikia wakulima wengi kwa kununua mazao yao kama malighafi katika kiwanda.

"Mpaka sasa tumeweza kuwafikia wakulima zaidi ya 1,500 katika Mkoa wa Pwani na Tanga ambapo kwa siku tunachakata zaidi ya tani 150 ya mahindi na kuyaongezea thamani kwa kuzalisha unga ambao tumekuwa tukiuza katika mikoa mbalimbali nchini," alisema Kimaro.

Mwenyekiti wa Bodi wa TADB, Ishmael Kasekwa, alisema ushirikiano kati ya TADB na AGRA umekuwa na mafanikio makubwa ambayo yanawezesha mageuzi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, hivyo Benki hiyo itaendelea kutoa mikopo ili kutekeleza azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda inafikiwa kupitia kilimo.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wapili kushoto), akipata maelezo kuhusu huduma za Benki ya NBC kutoka kwa Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki, Jonathan Bitababaje (kulia), alipotembelea banda la benki hiyo kwenye Maonyesho ya Sabasaba yaliyohitimishwa jijini Dar es Salaam juzi. Wanaofuatilia ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (katikati) na Mkurugenzi wa TANTRADE, Balozi Mteule, Edwin Rutageruka (kushoto). NBC ndio ilikuwa mdhamini mkuu wa maonyesho hayo. **MPIGAPICHA WETU**

# JKT mshindi wa jumla wa Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha huduma za bidhaa, teknolojia ya kilimo na mifugo katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) yaliyofikia kilele juzi.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo ya ushindi huo, Mwakilishi wa Mkuu wa JKT, Meja Josephat Yongo, alisema siri kubwa ya ushindi huo ni ubunifu na kufanya kazi kwa bidii kubwa.

"Siri kubwa ya ushindi wetu ni ubunifu na kufanya kazi kwa bidii sana, sisi JKT tunaangalia kwenye soko kunahitajika nini, wapi watu wanapata changamoto na sisi tunaigeuza kuwa fursa ya kuleta maendeleo kwenye makundi yote kwenye jamii," alisema Meja Yongo.

"Na tumekuwa tukishinda tuzo hizi kila mwaka na huwa tunachukua zaidi ya tatu. Tumeshinda leo, tunajipanga tena kuanzia sasa kwa ajili ya ushindi mwingine mwaka unaokuja."

Siri nyingine alisema ni namna ambavyo wanatoa huduma na kuzalisha bidhaa bora ambazo zinakidhi mahitaji ya kila kundi kuanzia la chini, la kati na la juu ambazo pia zinakidhi viwango vya soko la ndani na nje.

"Na kazi yetu ni malezi na mafunzo, na tuna kila kada, watu wenye teknolojia mbalimbali, kazi yao wakati wote ni kuwaza je, kesho tutakuwa wapi? Taifa na dunia kwa ujumla vinataka nini? Kwa hiyo sisi tukishajua nini kinahitajika, tunapambana kutafuta majibu, tunafanya hivyo kwa sababu bila kuwa na uchumi unaoeleweka hatuwezi kufika mbali," alisema Meja Yongo.

"Pia tunahamasisha zaidi katika kutengeneza ajira za watu. Na sisi kawaida yetu tunafanya kazi kwa bidii sana na matarajio ni kushinda makombe mengi zaidi, na tumekuwa tukijitahidi kuwafundisha vijana kuwa hivyo, kufanya kazi kwa bidii na kibunifu, kuzalisha kwa ubora si tu kwa kuangalia soko la ndani lakini na la dunia."

Aliwataka vijana kujiandaa kujifunza taaluma ambazo watajiajiri wenyewe badala ya kutegemea au kusubiri kuajiriwa.

"Sisi tumekuwa tukiwashauri sana na kuwajenga vijana namna ya kujiajiri wenyewe, tunataka wao ndio wawe mabosi kwenye shughuli zao kwa kuanzisha vitu vyao wenyewe wasisubiri kuajiriwa," alisema Meja Yongo.

Kwa upande wake meneja wa banda la JKT katika maonyesho hayo na ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko na Utafiti wa SUMA-JKT, Meja Peter Batimo, alisema jeshi hilo limekuwa mfano kupitia mambo mengi linaloyafanya na kwamba lengo lao ni kuendelea kuwa dira nchini.

"Na ndio maana hata ukiangalia katika maonyesho haya, kila mwaka sisi huwa tunashiriki na tunashinda, huwa tunakuwa wa kwanza kufungua kwenye maonyesho haya na tunakuwa wa mwisho kufunga," alisema Meja Batimo.

# NBC kinara taasisi za fedha Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC imeendelea kuwa kinara kwa mara ya nne mfululizo katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam, yaliyohitimishwa juzi katika mkoani Dar es Salaam kwa kutwaa ushindi wa kwanza katika kundi la taasisi za tedha.

Pamoja na kuwa mdhamini mkuu wa maonyesho hayo, benki hiyo ilikuwa mstari wa mbele katika kufanikisha ushiriki wa wadau wake katika maonyesho hayo wakiwamo wajasiriamali sambamba na kudhamini kliniki ya biashara iliyoandaliwa kwa ushirikiano Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE).

Akizungumza kwenye hafla ya ufungaji wa maonyesho hayo Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara kwa wateja wadogo na wa kati kutoka Benki ya NBC, Elvis Ndunguru, alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye maonyesho hayo umekuwa na tija kubwa kwa kuwa wamepata nafasi ya kuhudumia wateja wao sambamba kufungua fursa mpya za ushirikiano na taasisi mbalimbali likiwamo Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

"Mbali na kushirikiana na taasisi zaidi ya 16 katika kufanikisha kliniki ya biashara kwenye maonyesho haya, tumefanikiwa kufungua milango na taasisi nyingine zinazohudumia wajasiriamali na wafanyabiashara wanaochipukia ikiwamo SIDO ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza kuunganisha nguvu ili kwa pamoja tuwahudumie wadau hao muhimu kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda na biashara," alisema.

Aliongeza kuwa wakiwa kwenye maonyesho hayo benki hiyo ilipata fursa ya kupokea wageni mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali kama Makamu wa Rais Dk. Phillip Mpango aliyezindua maonyesho hayo, mawaziri mbalimbali pamoja na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleimani Abdulla, ambao pia waliiopongeza ipongeza benki hiyo kwa namna inavyoshiriki kuwasaidia wafanyabiashara nchini.

"Kama benki tumejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba tunayafanyia kazi maoni yote yaliyotolewa na viongozi waandamizi wa serikali pamoja na wateja wetu waliotutembelea lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba tunakusanya maoni yatayotuwezesha kubuni huduma zinazoendana na matarajio yao," alifafanua.

ama
ALHAMISI JULAI 15, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12



## NISHATI MPYA AINA YAKE KUTOKA UNACHOKISHANGAA MAKAZI ULIKO

Ukurasa 13



## Fahamu chanzo usiri kwa mwanamama mwenye VVU na anavyoangukia mateso

# Ufuatiliaji kinga Corona sasa unavyopamba moto serikalini

**Na Yasmine Protace**



Sehemu ya maandalizi ya kupimia corona Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam. **PICHA: YASMINE PROTACE**.

KATIKA kupambana na ugonjwa wa corona, jamii inatakiwa kuchukuwa hatua mbalimbali kujihami, mojwapo ni kunawa mikono kwa maji tiririka, kufanya mazoezi na kuvaa barakoa.

Hatua hizo zina mchango mkubwa katika kuuepuka ugonjwa huo. Serikali imekuwa ikitoa elimu kupitia njia mbalimbali kukabiliana nao.

Hivi karibuni serikali iliwataka viongozi wa ngazi ya mikoa na wilaya nchini kuhakikisha wanahamasisha wananchi kuchukua tahadhari na hatua zote kujikinga na ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alipokutana na viongozi wa Mkoa wa Dodoma na kutembelea linalozalisha hewa ya Oksijeni katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa, kukagua utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Waziri Gwajima anakiri wimbi la kwanza na la pili la ugonjwa wa Covid-19 bidhaa za tiba asili zilisaidia mapambano dhidi ya ugonjwa huo huku akisisitiza kuwa hazijafutwa.

Anasema, wananchi wavae barakoa, wawe na vitakasa mikono na kuwapo na maji tiririka kwenye maeneo yote yenye mkusanyiko na anaongeza kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan alivyosema Tanzania tayari ina wagonjwa kadhaa hivyo ni vyema kila mmoja akachukua tahadhari.

### WATENDAJI WAKUU SERIKALINI

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amwagiza Mkuu wa Kikosi cha Barabarani mkoani humo, kuhakikisha daladala zote zipakie abiria kulingana na idadi ya viti na hakuna abiria atakayesimama.

Mtaka anawataka mameneja wa masoko yote ya mkoa wa Dodoma, kuhakikisha maji tiririka yanakuwapo kwenye masoko yao, na kuvaliwa barakoa.

"Niwaombe wananchi wote kujilinda na kulinda wenzake, tuvae barakoa, tuepuke mikusanyiko isiyo na lazima, tubebe vitakasa mikono, tupunguze pia kugusana na kukumbatiana na kwenye nyumba za ibada tuepuke kushikana mikono, anasema Mtaka.

Pia serikali imeboresha miundombinu kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa ajili ya upimaji wa virusi vya Corona kwa wasafiri wanaoingia nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Profesa, Abel Makubi, wakati alipotembelea uwanja huo akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi(Sekta ya Uchukuzi) Gabriel Migire.

Makatibu Wakuu hao wakifika uwanja wa ndege kwa wa ajili ya kujionea maboresho yaliyofanywa kwenye uwanja huo ikiwamo zoezi la upimaji wa corona kwa wageni wanaoingia nchini. Aidha walitumia muda huo kujionea na kutatua changamoto mbalimbali.

Profesa Makubi amesema kuwa zoezi hilo limeanza muda sasa hapa nchini na kulingana na wasafiri kuongezeka hivyo serikali imeona ipo haja ya kuboresha miundombinu kila wakati ili kuendana na idadi ya ndege zinazoingia na kuepusha kero za huduma kwa wananchi.

"Suala hili la upimaji sio la sekta moja hivyo tumeona ni vyema kuja pamoja na Katibu Mkuu mwenzangu na kujionea ili tuweze kuboresha kwa upande wote sote.

"Sasa hivi maboresho makubwa yamefanyika ikiwamo upande wa kutoa majibu ambapo msafiri anapokuwa amelipia anaweza kupata majibu yake moja kwa moja kwenye email yake bila kuchelewa," anasema.

Aidha anasema, utolewaji wa majibu sasa umekuwa wa muda mfupi na abiria anaweza kutumiwa kwa email, bila kuhitaji kuchapisha cheti.

Profesa Makubi, anasema kuna umuhimu wa kipimo hicho cha haraka cha corona kwa msafiri kwa sababu kuwa na cheti' ambacho anakuja nacho msafiri, kwani mtu anaweza kupata maambukizi njiani au hakupima kama inavyotegemewa na hiyo inasaidia kuepuka maambukizi kwa wananchi wengine.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Gabriel Migire, anasema ziara hiyo wameweza kubaini changamoto za vifaa, wataalamu na huduma za kibenki ambapo wataalum wa uwanja huo wamewathibitishia kuzishughulikia na kuzipatia ufumbuzi.

Migire anasema, kuanzia Jumanne (juzi) walianza kufuatilia kuona kama changamoto zilizopo kwenye uwanja huo zimepata ufumbuzi ili kama kuna jambo la kufanya jitihada wao watalifanya kazi na kuagiza kuanza kupatia taarifa za vikao vya kila siku kutoka kwa wataalamu hao.

Ameahidi wizara yake kuendelea kuwa karibu na Wizara ya Afya ili kutatua kwa pamoja changamoto zilizobaki katika viwanja na kuelekeza ifanyike tathmini tena kabla ya Jumanne ya kukabili ongezeko zaidi ya wasafiri/watalii kwa siku za usoni.

MAZINGIRA

UNAIJUA JOTOARDHI?

# Nishati mpya aina yake kutoka unachokishangaa makazi uliko

- Mto Majimoto, Bonde la Ufa kuna umeme
- Megawati 200 TANESCO rasmi, 4,800 zaja

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MTU anapotamka 'joto la ardhi linabeba maana gani? Kitaalamu ni aina ya uvuguvugu unaozalishwa katikati ya 'ganda' na kiini au kitovu cha dunia na inasafiri kwenye mpitisho au msafara na kuhifadhiwa duniani.

Ni nishati yenye matumizi mtambuka; moja kwa moja na yasiyokuwa moja kwa moja, pia yanayotofautiana kulingana na kiwango cha joto kilichoko.

Matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi huanzia nyuzi joto 25 hadi 200 na kiwango hicho hutegemea aina ya mahitaji.

Kuna matumizi yasiyokuwa ya moja kwa moja yanayoanzia nyuzi joto 110 mpaka 300, ambayo yanaanzia kuzalishia umeme, nishati inayopatikana kupitia mvuke wa maji moto.

Hitaji la moja kwa moja lipo kwenye jotoardhi hasa kwenye kilimo kukausha mazao, kupasha joto kitalu nyumba, ufugaji samaki, utalii, viwandani na upashaji joto nyumba, hasa kwenye nchi zenye baridi kali.

Jotoardhi inapatikana katika maeneo mbalimbali duniani na hasa yaliyopitiwa na Bonde la Ufa na inadaiwa mara nyingi huambatana na majimoto.

Tanzania iko katika orodha ya mataifa yenye viashiria vya uwapo wa nishati katika maeneo mbalimbali. Imo ndani ya Bonde la Ufa la Afrika Mashariki na inadaiwa ina inapatikana katika maeneo 52 yenye viashiria hivyo.

Inaelezwa, kitaalamu Tanzania inatajwa kuwa na hazina ya zaidi ya megawati 5,000 za nishati hiyo ya jotoardhi zinazoweza kutumika.

### UENDELEZAJI WAKE

Taasisi ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), ni kampuni tanzu ya Shirika la Ugavi wa Umeme nchini (TANESCO), iliyopewa jukumu kusimamia maendeleo ya nishati yake kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Kato Kabaka, anasema mpaka mwaka 2018, kampuni ilishafanya utafiti katika maeneo saba, kati ya 52 yenye viashiria vya jotoardhi na kukusanya taarifa za kisayansi.

Anayataja kuwa ni; Songwe, Ngozi na Mbaka-Kyejo mkoani Mbeya, Luhoi mkoani Pwani, Ibadakuli mkoani Shinyanga, Kisaki mkoani Morogoro na Natroni mkoani Arusha.

Mhandisi Kabaka anasema, maelekezo ya serikali ni kwamba katika kuongeza uzalishaji nishati ya umeme nchini, TGDC imeelekezwa kutumia nishati jotoardhi kuzalisha megawati 200 za umeme ifikapo mwaka 2025, hivyo tayari wanaendelea na kazi hiyo.




Meneja Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji wa Nishati ya Jotoardhi, Mhandisi Kato Kabaka. **PICHA PICHA ZOTE:: NEBART MSOKWA**

"Tayari tumeshaanza kufanya utafiti wa uchorongaji wa visima katika maeneo matatu ambayo ni Ngozi na Mbaka-Kyejo mkoani Mbeya pamoja na Songwe mkoani Songwe.

"Tukishamaliza kuchoronga visima hivyo na kupata matokeo tunayoyahitaji, tutaendelea na uchorongaji wa visima kwa ajili ya uzalishaji," anasema Mhandisi Kabaka.

Anasema, uchorongaji visima kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa umeme umeanza katika chanzo kimoja cha Mbaka-Kyejo, ambako wameingia mkataba na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa gharama ya Sh. bilioni 1.1.

### MRADI MBAKA - KYEJO

Meneja Mradi wa kuchoronga visima vya Jotoardhi katika eneo la Mbaka-Kyejo, Albano Mahecha, anasema wanakusudia kuchoronga visima vitatu, kila kimoja kikiwa na kina mita 300.

Anasema kati ya kisima kimoja hadi kingine, kutakuwapo umbali wa mita 500 (nusu kilomitai) na vitakuwa katika muundo wa mstari ulionyooka, kufuata mpasuko wa mwamba. Ni visima vinavyochimbwa karibu na kilipo kiashiria, ambacho ni maji moto ya Mbaka-Kyejo.

Mahecha, ambaye ni Mjiolojia Mwandamizi, anasema wameanza na kisima kimoja na tayari wameshapata matokeo kuyakuta maji moto yenye nyuzi joto kati ya 65 na 70, katika kina cha mita 70 kati ya 300 zinazohitajika.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati) akiyashika maji moto, katika Kitongoji cha Majimoto Kata ya Nanyala, wilayani Mbozi mkoani Songwe. Ni mradi unaotarajiwa kuzalisha umeme megawati 35.

Anasema kabla ya kuchoronga visima, walianza kutafiti ardhini kwa kuangalia viashiria na kisha wakachoronga visima, ikiwa sehemu ya mwendelezo wa utafiti huo.

"Tunachokifanya hivi sasa ni utafiti wa chini ya ardhi 'drilling' (uchorongaji) wa visima ili kujiridhisha na uwapo wa nishati hiyo kama tulivyotarajia, pamoja na kuhuisha taarifa zingine zinazohusu uwapo wa nishati hii ya jotoardhi katika eneo hili," anasema Mhandisi Mahecha.

Anafafanua matarajio hayo, kwamba kazi hiyo itachukua muda mfupi kwa matarajio mwaka 2025 umeme unaotokana na nishati hiyo utakuwa unazalishwa kwenye eneo hilo, kutokana na kazi hiyo kufanywa kwa teknololjia ya kisasa zaidi.

### FAIDA ZILIZOKO

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TGDC, Mhandisi Shakilu Kajugusi, anasema nishati ya jotoardhi ni miongoni mwa nishati jadidifu ambazo ni rafiki wa mazingira na zikitumika ipasavyo zitasaidia kukabili uharibifu wa mazingira.

Vilevile, anasema kuna uzalishaji umeme kwa kutumia nishati hiyo ni gharama nafuu zaidi kuliko vyanzo vingine vya umeme, hivyo itasaidia kupunguza gharama za uzalishaji umeme ikiwa katika miongoni mwa vyanzo vyake vya uhakika.

Anasema, gharama ya uzalishaji umeme kwa kutumia nishati hiyo ni kubwa katika hatua za awali, kuanzia utafiti na uchimbaji, lakini uendeshaji wake ni nafuu.

"Pia nishati hii ni ya uhakika, endelevu na haiathiriwi na hali ya hewa, yaani kiwango cha umeme kinachozalishwa usiku na mchana ni kilekile, umeme huo hautegemei uwepo wa jua wala upepo," anasema Mhandisi Kajugusi.

Anasema, mradi wa uchorongaji visima wa eneo Mbaka-Kyejo, unatekelezwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa gharama Sh. bilioni 1.1 na utakapokamilika utakuwa wa kwanza wa uzalishaji wa umeme wa jotoardhi nchini.

Anasema, licha ya malengo yaliyopo ya megawati 200, uwezekano uliopo ni kuzalisha mpaka megawati 5,000, kutokana na hazina iliyopo.

### WAZIRI KALEMANI

Februari mwaka huu Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alifanya ziara katika eneo la Majimoto Songwe kukagua utekelezaji wa miradi ya jotoardhi.

Waziri alisema vyanzo vya nishati ya jotoardhi vilivyopo katika mikoa ya Mbeya na Songwe, vina uwezo wa kuzalisha megawati 165 za umeme, hivyo akaitaka TGDC kuwekeza nguvu kwenye vyanzo hivyo, vya Songwe, Ngozi na Mbaka-Kyejo mkoani Mbeya

Pia aliwawasisitiza kuendeleza utafiti kwenye vyanzo vya Natroni mkoani Arusha, Luhoi Pwani ili kufikisha Megawati 200 ifikapo 2025.

Alisema, pia serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme, ukiwamo wa Mwalimu Nyerere.

### ELIMU KWA WADAU

Ni aina ya uendelezaji nishati ulioambatana na utoaji elimu kwa wadau, ili kuhakikisha kunakuwapo uelewa wa kutosha kuhusu nishati hiyo na faida zake.

TGDC kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Mbeya, waliandaa mafunzo maalumu kwa wapasha habari hao kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe, ambayo yalijumuisha nadharia, kisha wakazuru eneo la Mradi wa Mbaka-Kyejo wilayani Rungwe, kushuhudia uhalisia wao uchorongaji visima vya kuzalisha wa nishati ya umeme.

Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya, Festo Sikagonamo, aliushauri uongozi wa TGDC kuongeza wigo wa elimu kwa wananchi, kwa kuyafikia makundi mbalimbali.



Sehemu ya mradi wa umeme wa joto ardhi

AFYA

## JICHO RASMI LA TACAIDS:

# Fahamu chanzo usiri kwa mwanamama mwenye VVU na anavyoangukia mateso

• Wadau kimataifa, bungeni, maofisa jamii, wataalamu...

**Na Augusta Njoji, aliyekuwa BAGAMOYO**

LICHA ya wanawake na wasichana kuongoza kupima na kupata huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi, bado wanakumbana na vikwazo vinavyochochea maambukizi mapya.

Miongoni mwa vikwazo hivyo ni kutokuwapo usawa wa kijinsia, unyanyapaa na ubaguzi, inayowasababisha wengi washindwe kuweka wazi hali za afya zao kwa wenza na jamii.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa linalopambana na UKIMWI (UNAIDS) mwaka jana, inaonyesha kundi hilo ndilo liko hatarini, kukiwapo wastani wa msichana mmoja kati ya wanne barani Afrika ana maambukizi ya Virusi vya Ukimwi(VVU).

Pia, tathmini ya taifa juu ya usawa wa kijinsia katika mwitikio wa udhibiti wa VVU iliyofanywa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Uwezeshaji wa Wanawake(UN-Women) mwaka jana, inasema asilimia 60 ya wanaoishi VVU nchini ni jinsia ya kike.

Ni hoja ya Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Lucas Kitula, katika mafunzo kwa wanahabari waandamizi kuhusu mwitikio wa Ukimwi katika mtazamo wa kijinsia, ili kuuondoa unyanyapaa na ubaguzi kwa wanaoishi na VVU na makundi yaliyo katika hatari kubwa ya kupata maambukizi mapya ya VVU, yaliyoratibiwa na TACAIDS.

Kitula anaitaka jamii iache matumizi ya lugha zinazoashiria ubaguzi na unyanyapaa kwa wanaoishi na VVU, kwani zinachangia baadhi ya kinamama kuacha kutumia dawa za kufubaza VVU (ARVs).

Anatoa mfano wa kuwapo kauli mbaya kwa kinamama watumiaji ARV, katika baadhi ya maeneo wametungiwa majina yasiyofaa, wanapoonekana katika vituo vya kuhudumia wenye VVU.

"Unyanyapaa umeonekana kuwapo katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye jamii, shuleni, mahali pa kazi, sehemu ya kutolea huduma, kwenye ngazi ya familia," anasema.

Anataja kashfa nyinginezo zinazojumuisha wenye VVU kunyooshewa vidole wanapoenda kuchukua dawa, husimamiwa kwa mafumbo na kashfa zenye majina tofauti.

"Vitendo vya kunyanyapaa au kumbagua mtu mwenye VVU kunasababisha hasa wanawake na wasichana kuhofia kuweka afya zao hadharani, ili wasitengwe na jamii au kusemwa maneno yasiyo faa, sasa hili lina hatari zaidi, kwa kuwa wenye maambukizi wataendelea kusambaza," anasema.




Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Lucas Kitula. **PICHA: AGUSTA NJOJI**

### MAENEO YA HUDUM A

Kitula anasema, katika baadhi ya vituo vya kuhudumia wahusika, kuna unyanyapaa wa kuchelewesha huduma ya taarifa, pia kuvujishwa, vyote vinasababisha wahitaji hao kukatishwa tamaa katika kufuata huduma hiyo muhimu kwa maisha na afya yake, badala yake anaacha kutumia dawa husika, hata akiingia katika madhara zaidi.

"Pia, inasababisha kukosa nauli na kutokwenda kufuata dawa na hivyo kuharibu utaratibu wa kupata dawa kwa wakati. Shuleni wanafunzi wakigundua mwenzao anaishi na VVU wanamtenga, wanamuita majina tofauti tofauti.

"Na hiyo inasababisha maendeleo yake darasani kushuka na maeneo ya kazini watu wanashindwa kupata stahiki zao kwa kuogopa kutengwa," anasema.

Aidha, anasema wanawake wengi wenye VVU wako katika hatari ya kufanyiwa ukatili pale wanapoweka wazi hali zao za maambukizi kwa jamii.

"Mfano katika Mkoa wa Lindi, kuna tathmini ilifanyika na kubaini wanawake wapo wazi kusema hali zao, lakini wanaposema wanaume hawaamini wanamuona iweje mwanamke awe na maambukizi kutokana na urembo wake.

"Pia wapo wengine wanaogopa kusema hali zao kisa watatengwa na jamii na hivyo kupelekea maambukizi kuendelea kusambaa," anasema Kitula.

### HALI NCHINI

Kitula anasema, utafiti wa hali ya UKIMWI nchini wa mwaka 2016/17, ilioonyesha wanawake wa umri kati ya miaka 45 hadi 49, wenye maambukizi ni asilimia 12 na wanaume asilimia 8.4, kwa wenye umri kati ya miaka 40 na 44.

Anasema ripoti hiyo inaonyesha upimaji unagusa asilimia 65.2 ya wenye umri wa miaka 15 na kuendelea waliripoti wamewahi kupima na kati yao asilimia 59.2 ni wanaume na wanawake asilimia 70.8.

Pia, asilimia 31.3 walisema wamepima kwa miezi 12 iliyopita; kati yao wanaume asilimia 29 na kinamama asilimia 33.5.

Akizungumzia tiba na matunzo, Kitula anasema wanawake kuanzia miaka 15 hadi-24, asilimia 59.4 walikuwa hawajui hali zao za VVU, na asilimia 35.8 walikuwa wanajua hali zao wakiwa kwenye matibabu.

Pia anasema wakati utafiti ulipokuwa unafanyika asilimia 4.8 walikuwa wanajua hali zao na hawakuwa kwenye matibabu, huku kutokuwapo usawa wa kijinsia una mchango mkubwa wa kimama kuambuikizwa zaidi VVU.

"Jamii zetu inaaminika anayefanya maamuzi kwenye familia ni baba na inaathiri hadi kwenye kufanya ngono salama. Mwanaume akisema hatutumii kondomu, wewe mwanamke huna cha kusema, unakosa uamuzi wa kufanya ngono salama," anaeleza.

### MIKAKATI ILIYOPO

Kitula anawahimiza wanahabari wajibu wa kusaidia kutoa elimu kwa jamii, ili iondokane na walakini huo akiuataja kuwa ni "unyanyapaa, ubaguzi na kukosekana usawa kijinsia."

Jumanne Issango, Mkurugenzi wa Habari na Uraghibishi wa TACAIDS, anasema utafiti zuaonyesha idadi ya maambukizi ya VVU yako kwa kiasi kikubwa kwa kinamama na vijana wa kike.

Ni hali inayoifanya serikali kuweka kipaumbele katika kushirikiana na wadau, ili kuwajengea uwezo walengwa kufikia malengo yaliyowekwa ya kumaliza VVU Ifikapo 2030.

Mratibu wa Programu za UKIMWI na jinsia UN-Women, Jacob Kayombo, anasema wanawake, wasichana wenye VVU na makundi maalum yanayotengwa, bado yanashindwa kupata huduma za msingi ikiwamo za kiafya.

Anasema wanakumbana na vikwazo katika kupata huduma, ikiwamo za kukosa nauli ya kuwafikisha panakopatikana huduma stahiki.

### KAMATI YA BUNGE

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Fatuma Toufiq, anasema tafiti nyingi zimebaini kuna uhusiano mkubwa kati ya maambukizi ya VVU na ukatili wa kijinsia.

"Kwa kiasi kikubwa maambukizi ya VVU miongoni mwa wasichana na wanawake yanachangiwa na kutokuwapo na usawa katika uhusiano wa kijinsia na ukatili, ukatili wa kijinsia ni kichoocheo cha maambukizi na madhara yanayotokana VVU," anasema.

Toufiq anasema, kuna kinamama walioambukizwa kutokana na ukatili wa kingono na bado wanashindwa kuongea.

"Mwanamke au msichana anapokwenda kukutana na mwenza wake hata atamwambia kuwa tuchukue tahadhari hawezi kuongea mwisho wa siku anakuja kuwa ni mwathirika," anasema.

Anasema, mwanamke akiweka wazi hali yake anakumbana na unyanyapaa mkubwa kwa kuwa jamii inamwangalia kwa jicho tofauti, lakini ni kinyume kwa mwanaume akiweka wazi hali ya maambukizi na kuomba radhi, anasamehewa kirahisi akiutaja ni mfumo dume.

### HALI ILIVYO MIKOANI

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Njombe, Alice Richard, anasema kuna baadhi ya walioambukizwa wanahofia kupoteza 'wateja', ikiwa wataweka wazi hali zao kiafya.

Pia, ofisa kama huyo kutoka mkoa Rukwa, Aziza Kalyatila, anasema kutokana na wanawake na wasichana kwenye eneo hilo kuwa na uchumi mdogo, wanashindwa kufikia vituo vya afya na kupata huduma stahiki.

AFYA

## LICHA MORO KUFIKIA 'VIFO SIFURI'...

# Madereva na ajali za vilevi, doa kuu linaloendeleza madhara kwa umma

Na Christina Haule, Morogoro

## • RPC Musilimu asimulia vita vyao

VIFO vya ajali za barabarani kutokana na ulevi mkoani Morogoro vinatajwa sasa kupungua, kutoka vifo 18 mwaka 2018 hadi kufika mwaka jana, hakuna hata kimoja.

Kamanda wa Polisi Mkoa humo, Fortunatus Musilimu, anasema ni zao la kutolewa elimu, kazi inayoendelea kuitoa kwa madereva wa mabasi, magari madogo, makubwa, ya mizigo na pikipiki sambamba na abiria kutambua haki zao, kwa kuipa polisi taarifa ya kuwapo madereva wenye tabia hiyo.

Kamanda Musilimu anasema, mwaka 2018 kulitokea jumla ya vifo 80 vya ajali na yapo yatokanayo na ulevi wa madereva. Walikuwapo majeruhi 123 watokanao na ajali 68.

Anasema mwaka uliofuata kulikuwapo vifo 67 vya ajali na kimoja pekee ndicho cha ulevi vikitokana na ajali 75, iliyoacha majeruhi 78.

Kamanda huyo anasema, mwaka jana ulikuwa na vifo 57 vya ajali za barabarani na hakuna kitokanacho na ulevi; majeruhi wako 88, watokanao na ajali 54.

### MADEREVA NA ULEVI

Ndani ya muda huo, Kamanda Muslimu anasema, madereva waliobainika na matukio ya ulevi mwaka 2019 baada ya kupimwa na kifaa maalum kitwacho 'Alchotester', jumla yao ni 43. Wengi wanatokana na malori, wapanda pikipiki saba, baiskeli (4) na watembea kwa miguu wawili.

Anasema, wakati ajali za mwaka jana ziliwaangukia madereva 22 wa magari, sita wa pikipiki 6, wapanda baiskeli wawili, watembea kwa miguu watatu waliogundulika kulewa baada ya kupimwa na watuhumiwa 33 walishikiliwa kwa dai la ulevi.

Kwa mujibu wa Kamanda Muslimu, madereva hutumia vilevi, huku Sheria Namba 49 cha Makosa ya Usalama Barabarani kinaainisha dereva wa gari hapaswi kukutwa na kilevi kilichozidi milimita 80, kutoka wastani wa milimita 100 za damu mwilini mwake.

Anafafanua kuwa, kisheria za usalama barabara zinawataka madereva wa magari ya abiria na mizigo, hapaswi kuwa na kiwango



Enock Mbago mmoja wa majeruhi akiwa amelazwa katika Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro baada ya kupata ajali iliyomsababishia kuvunjika kwa mguu. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

chochote cha kilevi mwilini, kwa sababu anaweza wakashindwa kuwa na uamuzi sahihi, anapokuwa amelewa.

### SSP MICHAEL STEPHEN

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro (RTO) Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Michael Stephen, anaiomba serikali kuona umuhimu wa kuwekea vipimo vya ulevi wa dawa za kulevya, kwenye vituo vikuu vya polisi kila mkoa.

Anasema, hilo linarahisisha upimaji wa vilevi, kwani hadi sasa hivyo hupatikana katika maabara ya kipolisi na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) jijini, Dar es Salaam pekee na wamebaini kuwapo matukio ya ulevi wa madereva, pindo polisi wanapoendesha operesheni zao kila mara.

SSP Stephen, anataja baadhi ya maeneo mkoani waliofanya operesheni hizo ni katika Mansipaa ya Morogoro, zikiwamo stendi za magari na kituo kikuu cha mabasi ya mikoani- Msamvu na vingine vidogo ndani ya Mansipaa ya Morogoro, wakitumia kipimo cha ulevi dhidi ya dereva, pindi walipomshuku.

Kamanda wa Usafiri Stephen, anasema udhibiti wa ulevi barabarani, ni zao la hatia kongwe kutoka Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka ya 1973.

Anasema mwaka 2006, serikali ilisambaza vifaa maalum vya kupima kiwango cha ulevi kwa dereva washukiwa, wanaopuliza pumzi zao mdomoni kwenye na kifaa hicho na kutoa majibu ya ama kuwapo au la walevi.

Kamanda Stephen anasema, madhara madhara ya ulevi yanajumuisha uendeshaji wa gari ikiwa hatarani na ajali na inapogundulika hilo, moja ya hatua za kisheria ni kumfikisha mtuhumiwa mahakamani.

Wito wake, anawataka madereva kuacha kuendesha vyombo vya moto huku wakiwa wamelewa, bali watumie mwene nia ya hilo alitumie nje ya muda wa kazi.

Pia, anawaasa wafanyabiashara za vileo, kutokuwa tayari kutomhudumia dereva aliyefika na gari na yuko katika kiwango cha ulevi uliopitiliza, vivyo hivyo anawaomba madereva wasitumie pombe muda wa kazi.

"Wapo madereva hujikita kwenye ulevi na kusahau kuwa wameenda na chombo cha moto kwenye starehe zao na kuondoka wakiendesha na kusababisha ajali, wakipimwa hukutwa na mililita 200 za kilevi kwenye mililita 100 za damu mwilini.

### PIKIPIKI JE?

Kamanda Stephen, anasema waendesha pikipiki za biashara maarufu bodaboda, ni wasababishaji ajali kutokana na uzembe, pia kubeba abiria wa ziada maarufu 'mishikaki ajali ambayo mara nyingi huwa inasababishwa na abiria kwa kulazimisha kubebwa mishkaki huku wakiwa hawajavaa kofia ngumu.

Anataja baadhi ya makosa ya waendesha pikipiki, hata kusababisha ajali yanajumuisha kulipita gari au chombo kingine cha moto katika upande wa usio sahihi kisheria, kubeba abiria zaidi ya mmoja, ulevi na kutovaa kofia ngumu.

Huku akiwaonya waendesha pikipiki hao kuwa mkondo wa sheria utawakabili, anawataka wazingatie sheria za barabarani, adhabu za kisheria inapothibitika inajumuisha faini na kifungo.

"Upo uzembe ambao hufanywa na dereva mmoja wa pikipiki kwa kuamua kuingia mkataba na wamiliki zaidi ya mmoja, pengine hata wanne na baadaye, yeye anabaki na pikipiki moja na zingine kuwapa madereva wengine aliowafundisha kuendesha usiku mmoja, ambao hawawezi.

"Nao huingia barabarani na kusababisha ajali na baada ya kukamatwa mmiliki huja na kudai huyo sio aliyempa pikipiki," anafafanua.

Ushauri wake ni kwa wamiliki wa pikipiki kujenga tabia ya kukagua miliki za pikipiki zao kwa walioingia nao mikataba, hali inayosaidia kupunguza ajali barabarani.

### SIMULIZI ZA MAJERUHI

Enock Mbago, majeruhi aliyewahi kupata ajali ya gari na kupata ulemavu, anasema yalimkuta Februari mwaka huu, eneo la Kihonda Maghorofani, mjini Morogoro alipokuwa anampeleka mtoto shuleni na hadi sasa anaendelea na matibabu hospitalini Muhimbili, Dar es Salaam.

Mbago, ambaye mguu wake umewekewa chuma na bado haujapona, anasimulia mkasa wake akiwa na pikipiki dereva wa gari alihamia upande wake baada ya kuyazidi mbele magari matatu kwa pamoja na kuyumba kwenye kivuko cha waenda kwa miguu, kisha kumgonga yeye akiwa na bodaboda upande wa kulia.

Rai yake ni kwamba, serikali imsaidie katika matibabu, pia mahitaji ya kifamilia, kwa sababu gari iliyomgonga ni ya serikali na yeye alikuwa anatafuta na kulisha familia yake kwa kazi ya kuendesha bodaboda, akilalamika familia yake sasa iko matesonia.

Mbunge wa Viti Maalum wa Watu Wenye Ulemavu, Fatma Toufiq, anasema jamii inapaswa kutambua umuhimu wa kutii sheria na kanuni za usalama barabarani, hasa akiwaangazia madereva wanaoshindwa kuona umuhimu wa alama ya kivuko cha wanaoenda kwa miguu, hata kuwagonga wasiohusika na kusababisha madhara na hata matukio ya vifo.

Anakiri, naye alishawahi kupatwa na ajali na kuumia mguuni na kupata ulemavu ambao hakutarajia, baada ya dereva aliyekuwa akiendesha gari, kushindwa kulimudu akaishia kugongana uso kwa uso katika gari lake.





## Ndugai afagiliwa kwa uchangiaji maendeleo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BARAZA la Mamlaka ya Mji wa Kongwa mkoani Dodoma limewataka wananchi kuunga mkono jitihada za Spika wa Bunge, Job Ndugai, katika kuchangia miradi ya maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, White Zuberi, katika mkutano wa baraza hilo wa kujadili taarifa ya robo ya nne ya mwaka wa fedha 2020/21. Alisema Ndugai amewezesha miradi mbalimbali ambayo ni kichocheo cha maendeleo kwa wananchi.

"Miradi hiyo kuwa ni pamoja na taa za barabarani ambazo zimesaidia kupunguza wizi nyakati za usiku, huduma ya majisafi kutoka visima vya Ibwaga na VETA, upanuzi wa Hospitali ya Wilaya, ujenzi wa mabweni ya Kongwa Sekondari, ujenzi wa maabara Shule ya Sekondari Mnyakongo, uboreshaji wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha changarawe."

"Usambazaji wa nguzo za umeme katika vitongoji vya Viganga, Mnyakongo Kisimani, Mnase, Barabara ya Dodoma na Chimlata," alisema.

Alisema juhudi hizo zinatakiwa kuungwa mkono na wananchi ili kuchochea maendeleo ya wilaya hiyo kutokana na kuwa na miundombinu yenye kunufaisha wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Mamlaka hiyo, Onesmo Semundi, alisema watashirikiana na Halmashauri ya Wilaya kuhakikisha makusanyo yanarejeshwa kwa wakati, ili kuendesha kwa ufanisi shughuli za mamlaka hiyo.

Katibu wa Mamlaka hiyo, Geofrey Kalatunga alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, Sh. milioni 70.3 zilipokelewa sawa na asilimia 86.81 ya fedha zilizoidhinishwa na kati yake Sh. milioni 43.9 zimetumika kwa matumizi ya kawaida huku Sh. milioni 15.8 zikitumika kwa miradi ya maendeleo. Alisema katika kipindi hicho mamlaka hiyo ilikusanya Sh. milioni 34.9 na kuziwasilisha halmashauri. Alifafanua robo ya nne ya mwaka, mamlaka hiyo imepokea Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya maboresho ya miradi ya elimu na afya.

# Miundombinu zaidi yawekwa mji wa serikali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MJI wa Serikali Mtumba jijini Dodoma umeendelea kuwekewa miundombinu ya kisasa itakayosaidia na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi wanaofika katika ofisi zote zilizopo katika eneo hilo.

Katibu wa Kikosi Kazi cha Taifa cha Kuratibu Mpango wa Serikali wa Kuhamia Dodoma na Uratibu wa Ujenzi wa Mji wa Serikali unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Meshack Bandawe, aliyasema hayo juzi alipoongoza kikao cha timu ya wataalamu kukagua miundombinu mbalimbali.

Timu hiyo ilikagua miundombinu ya majisafi na majitaka, umeme, mawasiliano, usalama, ujenzi wa majengo marefu ya wizara awamu ya pili, barabara za lami, zimamoto na uokoaji, gesi na upandaji miti ya matunda.

Akizungumza ukaguzi huo, Bandawe alisema mji huo ambao utakuwa wa kisasa kutokana na miundombinu iliyojengwa na inayoendelea kujengwa.

"Kuna barabara za lami, uwekaji taa za barabarani, majengo ya kisasa na miundombinu mingine itakayoufanya mji huu kuwa na mvuto wa kipekee kama ilivyo dhamira ya serikali," alisema.

Aidha, alisema miundombinu mingine itawekwa chini ya ardhi ili kuweka mandhari ya mji huo kuwa wa kisasa na kuvutia.

Kuhusu ujenzi wa barabara za lami, Bandawe alisema kazi hiyo inaendelea na imefikia zaidi ya asilimia 70, na kazi ya kuweka miundombinu mingine inaendelea kama ilivyopangwa.

"Na ujenzi wa Mji wa Serikali awamu ya pili unatarajiwa kuhusisha ujenzi wa majengo makubwa ya ghorofa kwa kila wizara, kutapandwa miti ya aina mbalimbali ya matunda," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya kifedha ya K Finance, Devotha Minzi (wa pili kushoto), baada ya kuzindua rasmi ofisi ya taasisi hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mrajisi aagiza mfumo wa udhibiti TCDC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MRAJIS wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, ameitaka Menejimenti Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), kuweka mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuzuia vihatarishi vitakavyosababisha wasifikie malengo. Mifumo hiyo ni pamoja na kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo kwenye utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Dk. Benson Ndiege aliyasema hayo alipokuwa akifungua mafunzo kwa kamati ya ukaguzi na wajumbe wa menejimenti ya tume, jijini hapa.

Alisema jukumu la menejimenti ni kuhakikisha kuwa kazi zinatekelezwa kwa kuzingatia malengo ya tume, mipango na mikakati ya utekelezaji wa majukumu inazingatiwa na inatekelezwa ipasavyo na kunakuwa na matumizi mazuri ya rasilimali za tume.

"Kamati ya ukaguzi ni chombo muhimu chenye jukumu la kusimamia kazi za ukaguzi wa ndani kiufundi na kumshauri afisa masuuli kuhusu udhibiti wa ndani, menejimenti ya vihatarishi na utawala bora ili kuiwezesha tume kufikia malengo yake."

"Ili kamati iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ni muhimu kamati ifanye kazi kwa weledi na ufanisi. Hivyo, mafunzo haya ninayoyazindua leo yanatarajiwa kuisaidia kamati kuongeza weledi na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake," alisema. Hata hivyo, alisema mafunzo hayo yataiwezesha menejimenti ya tume kuelewa majukumu ya kamati ya ukaguzi na pia kujifunza wajibu wake kuhusu utekelezaji wa ushauri na mapendekezo yanayotolewa na ya kamati ya ukaguzi.

Alisema ili kazi ya kamati ya ukaguzi ya kushauri iwe nyepesi, ni jukumu la menejimenti ya tume kuhakikisha kuwa inaweka mifumo toshelevu.

Mrajis huyo alisema serikali imedhamiria kwa dhati kuendeleza na kuimarisha vyama vya ushirika ili kuleta tija kwa wanachama na hatimaye kuijenga Tanzania yenye uchumi wa kati na wa viwanda kupitia vyama vya ushirika.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ya TCDC, Evance Assenga, alisema wanachofanya katika kamati hiyo ni kupitia taarifa za mkaguzi wa ndani na taarifa ya mkaguzi wa nje pamoja na kushauri katika eneo la utawala bora.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Namba 30 inataka taasisi kuwa na kamati ya ukaguzi. Nipende kukuthibitishia kwamba ofisi yako tayari ina kamati ya ukaguzi na inaendelea mwaka wa tatu na inafanya vizuri."

"Kwa mujibu wa sheria inatutaka tukutane mara nne kwa mwaka na haya yote tumeweza kuyatimiza mara zote nne kwa mwaka," alisema.



# Wazazi wasisitizwa chanjo saratani ya mlango wa kizazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi wametakiwa kuridhia na kuhamasisha watoto wa kike kupata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi ambayo inadaiwa imeongezeka na kuwa chanzo kikubwa cha vifo kwa wanawake nchini.

Wito huo ulitolewa jana jijini Mbeya na Meneja wa Mradi wa Huduma Jumuishi za Chanjo ya Kinga ya Saratani ya Mlango wa Kizazi, ulioko chini ya Shirika la Jhpeogo kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Maryrose Gittas, wakati wa mafunzo maalumu kwa waandishi wa habari wa mkoa wa Mbeya.

Mafunzo hayo yalikuwa yanalenga kuwajengea uwezo wanahabari wa mkoa wa Mbeya kuhusu huduma za chanjo ya kuzuia ugonjwa huo ambayo yaliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Shirika hilo la Jhpeogo na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema kumekuwapo na tatizo la baadhi ya wazazi kuwazuia watoto wao kuchanjwa kutokana na kuwa na elimu ndogo kuhusu umuhimu wa chanjo hiyo na kwamba ili kukabiliana na tatizo hilo, wazazi wanatakiwa kupewa elimu juu ya kutosha.

Gittas alisema tatizo la saratani ya mlango wa kizazi ni tishio kwa wanawake nchini na hivyo ni lazima juhudi za makusudi zichukuliwe ili kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema zaidi ya asilimia 40 ya wanawake wanaolazwa katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road ya Dar es Salaam huwa ni wale waliogunduliwa kuwa na saratani ya mlango wa kizazi hali ambayo alisema ni hatari.

"Tunachoshukuru Mungu ni kwamba saratani hii ni tofauti na ya matiti. Hii inatibika kirahisi endapo mgonjwa atagundulika mapema kuwa na maambukizi na ni saratani ambayo inazuilika kwa chanjo tofauti na ya matiti," anasema Dk. Gittas.

Alisema kwa sasa serikali pamoja na wadau mbalimbali wanatakiwa kushirikiana kuhamasisha jamii ili kila Mtanzania ashiriki kuwaokoa mabinti na janga hilo.

Mratibu wa Chanjo wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Danford Barnaba, alisema kwa mwaka 2020, mkoa huo ulikusudia kuwachanja wasichana 24,026 lakini waliochanjwa dozi ya kwanza walijitokeza 16,263 huku wasichana 7,763 wakikosa kuchanjwa.

Alisema sababu nyingine ya wasichana wengi kutochanjwa ni kukosekana kwa mawasiliano mazuri kati ya vituo vya afya na shule kwa maelezo kuwa asilimia kubwa ya wasichana wanaofikisha umri wa miaka 14 wanakuwa bado wako shuleni, hivyo kutosajiliwa.

Pia alisema katika baadhi ya maeneo usajili wa wasichana hao huchelewa kufanyika na hivyo muda wa kuchanjwa unapofika wanakuwa tayari wengine wamehitimu masomo na kurudi majumbani ama kufaulu na kupangiwa shule za sekondari za mbali na maeneo yao ya awali.

"Lakini tatizo hili si kwa mkoa wa Mbeya pekee bali ni kwa Tanzania nzima maana pamoja na kuonekana kuwa tulikuwa tumechanja wachache, tulishika nafasi ya nne kitaifa tukitanguliwa na Njombe, Kilimanjaro na Dar es Salaam," alisema Dk. Barnaba.

Alisema mikoa mingine iliyofanya vibaya ukiwamo mkoa Songwe na Iringa ambayo haikufikia hata nusu kwa maelezo kuwa Songwe walifikia asilimia 40 na ndio walioshika mkia huku Iringa wakifikia asilimia 46.

Alisema ili kukabiliana na tatizo la saratani ya mlango wa kizazi ni lazima elimu itolewe vya kutosha kuhusu chanjo ili kila msichana anayefikisha umri wa miaka 14 achanjwe dozi zote mbili na wanawake wenye umri kati ya miaka 35 na 50 wanatakiwa wawahi kufanya uchunguzi ili kubaini kama wana dalili za awali.

Njia za kuepuka saratani hiyo, alisema ni wasichana kubadili tabia kwa kuepuka kuwa na wapenzi wengi, kuepuka ngono katika umri mdogo, kuepuka kuvuta sigara na kuepuka kubeba mimba katika umri mdogo.



Baadhi ya wakulima wa Kijiji cha Chibila, katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe, wakiwa wamenyanyua mahindi juu wakati walipotembelewa na maofisa wa Taasisi ya HRNS waliowawezesha elimu ya kilimo hifadhi, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Jiji lakamilisha ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imesema tayari imekamilisha mradi mpya wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa asilimia 90 katika Shule ya Sekondari Iduda kwa ajili ya uanzishwaji wa kidato cha tano na sita katika mwaka wa masomo 2021/22.

Meya wa Jiji hilo, Dormohamed Issa, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo ambapo alisema ujenzi wa shule hiyo ni sehemu ya mikakati ya halmashauri hiyo kuboresha sekta ya elimu.

Alisema fedha za ujenzi wa mradi huo zilitokana na Mfuko wa Jimbo na kwamba msimamizi mkuu wa mradi huo ni Halmashauri ya Jiji na kwamba kwa sasa wanaendelea na ukamilishaji wa baadhi ya majengo pamoja na miundombinu mingine.

"Tutahakikisha miundombinu yote muhimu inakamilika kwa wakati yakiwamo mabweni, vyoo na bwalo, miundombinu mingine kama vyumba vya madarasa tayari tumekamilisha vizuri na mbunge wa jimbo letu, Dk. Tulia Akson, ametusaidia pia," alisema Dormohamed.

Fundi Mkuu wa Mradi huo, Froid Kibona, alisema baada ya kumalizika kwa ujenzi wa madarasa hayo, kinachoendelea kwa sasa ni kuanza kwa ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike.

Alisema wanaanza na mabweni ya wanafunzi wa kike kutokana na kundi hilo kukabiliwa na matatizo mengi tofauti na wa kiume ambao ujenzi wa mabweni yao utafanyika bajeti ya mwaka ujao wa fedha kutokana na maelekezo aliyopewa.

Ujenzi wa maabara za kisasa na kuboresha miundombinu ya vyumba vya madarasa ni mkakati mwingine ambao unatajwa na halmashauri hiyo katika kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

# Ataja sababu kushamiri kwa rushwa kwenye huduma

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TATIZO la rushwa kwenye huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi mkoani Mbeya bado ni tatizo kutokana na taarifa nyingi kutowasilishwa na wananchi katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Denis Manumbu, alipokuwa anatoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Aprili mpaka Juni mwaka huu.

Manumbu alisema katika kipindi cha miezi mitatu taasisi hiyo ilipokea taarifa 157 zinazohusiana na tuhuma za rushwa na makosa mengine yanayofanana na rushwa na kwamba taarifa hizo zilizihusu taasisi mbalimbali za umma na watu binafsi.

Alisema kati ya taarifa hizo 37 zilikuwa zinazihusu halmashauri mbalimbali za mkoa huo, 29 zilikuwa zinawahusu wafanyabiashara, 19 zilikuwa zinahusu idara ya ardhi na taarifa 12 zilikuwa zinahusu idara ya elimu.

Pia alisema taarifa 11 zilikuwa zinahusu Mahakama, taarifa 11 zilikuwa zinahusu mashirika ya umma, taarifa 10 zilikuwa zinalihusu Jeshi la Polisi, taarifa nne zilikuwa zinavihusu vyama vya ushirika, taasisi za fedha taarifa tatu, Sekta ya Afya taarifa tatu na Sekta ya Maji taarifa tatu.

Vilevile alisema taarifa mbili zilikuwa zinaihusu sekta ya kilimo, jeshi la akiba taarifa mbili, michezo taarifa mbili, mawasiliano taarifa moja, maliasili taarifa tatu, mifugo taarifa moja na taarifa zilizohamishiwa idara nyingine moja.

"Lakini kwa upande wa mashtaka, katika kipindi hicho cha miezi mitatu, tumefungua kesi mpya nne mahakamani kwa makosa mbalimbali na kesi 22 zilizokuwa zinaendelea mahakamani bado tuliendelea nazo kwa hatua mbalimbali," alisema Manumbu.

Katika hatua nyingine, Manumbu alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbalimbali juu ya kukabiliana na vitendo vya rushwa ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambazo zina klabu za wapinga rushwa pamoja na viongozi mbalimbali.

Pia alisema taasisi hiyo ilifanya ufuatiliaji wa miradi 10 ya maendeleo iliyokuwa ikitekelezwa mkoani hapa yenye thamani ya Sh. bilioni 8.17 ikiwamo ya sekta za elimu, afya na maji na kuishauri serikali kutokana na udhaifu uliobainika.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Gregory Emmanuel, alisema katika kipindi cha miezi mitatu TAKUKURU ilisaidia halmashauri hiyo kukabiliana na vitendo vya rushwa kwa kutoa elimu kwa watendaji mbalimbali wakiwamo wa kata na mitaa pamoja na madiwani.

Pia alisema taasisi hiyo iliwasaidia kudhibiti upotevu wa mapato kutokana na ukusanyaji uliokuwa unafanywa na watendaji kwa kutumia mashine za kielektroniki yaani POS.

"Lakini walitusaidia kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha, serikali imetupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo maofisa wa TAKUKURU waliikagua na kutushauri," alisema Gregory.



## Ripoti uchaguzi yatua kwa Rais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imekabidhi Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, huko Ikulu jijini Zanzibar.

Akikabidhi ripoti hiyo juzi, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, alisema ripoti hiyo imegawanyika katika sura saba na imezingatia hatua za mzunguko mzima wa uchaguzi, hivyo imezingatia hali ilivyokuwa kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi.

Mwenyekiti huyo alitoa shukrani kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kugharamia uchaguzi huo kwa asilimia mia na fedha zote kupatikana kwa wakati mwafaka.

Alisema hatua hiyo ya serikali ndiyo iliyowezesha tume kuendesha na kusimamia uchaguzi huo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mwenyekiti huyo alitoa shukrani kwa viongozi na watu wote waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Jaji Hamid alimweleza Rais Mwinyi kwamba uchaguzi huo ulifanyika kama ulivyopangwa bila ya kujitokeza hitilafu yoyote iliyosababisha kurejewa au kufunguliwa mashtaka ya kupinga matokeo.

Alisema kura ya mapema ilifanyika kwa mara ya kwanza na iliwarahisishia walengwa waliotajwa katika Sheria ya Uchaguzi kufanya kazi siku ya uchaguzi wa pamoja kwa ufanisi zaidi.

Alisema tume imewapata wataalamu wazawa waliofanikiwa kutengeneza mfumo mpya wa uandikishaji wa kisasa wa TEHAMA pamoja na kutayarisha mifumo mingine ya uchaguzi iliyoiwezesha tume kutekeleza uchaguzi kwa usiri na kwa ufanisi bila ya kuingiliwa.

Mwenyekiti huyo alisema tume ilichapisha kura zilizotumika katika Uchaguzi Mkuu Zanzibar na kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar tume ilikamilisha kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi ndani ya saa 24 baada ya upigaji kura kukamilika.

Mwenyekiti huyo aliyefuatana na wajumbe wake, alitumia fursa hiyo kumweleza Rais Mwinyi baadhi ya vikwazo vilivyowakabili.

Ripoti hiyo imekabidhiwa kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Mwaka 2017, kinachotaka kila unapomalizika Uchaguzi Mkuu, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inatakiwa kutayarisha ripoti na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya miezi 12.

Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema kuna kila sababu ya kutoa pongezi kwa wadau wote wa uchaguzi wakiwamo tume husika, vyombo vya ulinzi na usalama, Asasi za Kiraia na wananchi wote kwa ujumla.

"Ninachukua fursa hii ya pekee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Tume ya Uchaguzi na wadau wote wa uchaguzi kutokana na zoezi kwenda vyema," Dk. Mwinyi alisifu.

# Mbaroni kwa tuhuma vyeti feki vya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) inawashikilia watu 11 kwa tuhuma za kutengeneza vyeti bandia vyenye matokeo ya upimaji wa ugonjwa wa corona kwa wasafiri.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Ahmed Khamis Makarani, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mnazimmoja Mjini Unguja.

Alisema watu hao wanatuhumiwa kuwatoza fedha wasafiri na kuwatengenezea vyeti bandia vya corona bila ya kuwafanyia vipimo ili wapate kusafiri. Alisema kwa kutengeneza vyeti hivyo, watu hao walikuwa wakijipatia mali fedha kwa njia ya udanganyifu na kusababisha kuitia hasara serikali zaidi ya Dola za Marekani 50,000.

Mkurugenzi huyo aliwataja watu hao kuwa ni pamoja na Rashid Saleh (32), mkazi wa Michenzani anayefanya kazi katika taasisi ya kusaidia yatima; Peter Masika Wafula (41), raia wa Kenya anaishi kwa Mchina, akifanya kazi katika hospitali binafsi ya Al Rahma.

Wingine ni: Hassan Vuai Hassan (41), mkazi wa Kwarara na mfanyakazi wa Wizara ya Afya (Idara ya Maabara), Yassir Said Ali (27), mkazi wa Tomondo na mfanyakazi wa kujitolea ZACP katika Kitengo cha Covid-19; Jamal Abbas Abdalla (38), mkazi wa Kilimani na mfanyakazi wa uwanja wa ndege; Abdalla Mohammed Juma (25), mfanyabiashara katika Sekta ya Utalii.

Asya Gharib Haji (39), mkazi wa Mpendae na mfanyakazi wa Wizara ya Afya (Maabara); Salum Haroub Amour (24), mkazi wa Miembeni na mfanyakazi wa Bohari Maruhubi; Arafa Abdulhakim Muhsin (30), mfanyakazi wa Wizara ya Afya (Kitengo cha Covid-19); Mbarouk Khamis Ali (43), mkazi wa Masingini na mfanyakazi wa Wizara ya Afya (Maabara); na Hussein Ame Haji, mfanyakazi wa Kitengo cha Covid-19 makao makuu.

Alitaja idadi ya waliopewa vyeti feki vya corona kuwa ni 548, vyeti ambavyo wamepewa wasafiri waliotoka Zanzibar kwenda sehemu mbalimbali duniani.

"Kwa bahati mbaya sana, katika idadi ya waliopewa vyeti kuthibitisha kuwa wamepimwa corona, inajumuisha baadhi ya viongozi wa juu serikalini," alibainisha.

Alisema watu hao ni wafanyakazi katika taasisi mbalimbali ikiwamo za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na taasisi binafsi ambao kwa pamoja wanaingia katika mfumo wa vyeti vya Covid-19 uliokuwa halali na kuuvunja mfumo mzima na kuipata alama ya siri ya kutengeneza vyeti hivyo.

"Vyeti hivyo wakipita uwanja wa ndege vina alama inayoweza kusoma kuonyesha kuwa cheti hicho ni halali wakati vyeti hivyo si halali kutokana na kuichezea alama hiyo huku kwa maslahi yao binafsi bila ya kujali athari kubwa wanayoipatia nchi," alisema.

Aliongeza: "Mtu anapatiwa cheti hapa anaondoka nacho anapofika nje ya nchi, akipimwa akionekana ana tatizo, inaonekana vifaa vya Zanzibar pengine feki au siyo salama na havina uwezo na kiwango cha kugundua tatizo hilo."

Mkurugenzi huyo alisema kitendo hicho cha kutoa vyeti feki kinaitia doa Serikali ya Zanzibar katika nchi mbalimbali duniani kwa kuonekana vifaa vya kuchunguza maradhi hayo siyo vya uhakika.



Katibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hassan Makeme (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar jana, kuhusu wagonjwa na watu wote wanaofika hospitalini hapo, kuhakikisha kuwa wanavaa barakoa la sivyo hawatoruhusiwa. Kushoto ni Mkurugenzi Huduma za Tiba wa hospitali hiyo, Dk. Abrahman Khalfan na Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga, Haji Mnyonge Pandu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zanzibar kudumisha ushirikiano na Oman

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar itaendeleza ushirikiano wake wa kihistoria na Oman ikiwamo kibiashara, kiuchumi na kijamii.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu jijini Zanzibar wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi Mdogo wa Oman anayefanya kazi zake Zanzibar, Said Salim Alsinawi, aliyefika Ikulu kwa ajili ya kujitambulisha kwa Rais.

Katika mazungumzo hayo, Rais Mwinyi alimkaribisha Zanzibar Balozi Alsinawi na kumhakikishia Serikali ya Zanzibar pamoja na wananchi wake wote wataendeleza uhusiano na ushirikiano na Oman ambao ni wa kihistoria.

Rais Mwinyi alimhakikishia Balozi huyo mdogo wa Oman kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendeleza uhusiano na ushirikiano na Oman na inathamini juhudi za ubalozi huo katika kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana na Oman na inatambua hatua na juhudi mbalimbali inazozichukua Serikali ya Oman katika kuiunga mkono Zanzibar hivi sasa ikiwa ni pamoja na kusaidia ujenzi wa Jumba la Beit Al Jaib pamoja na Jumba la Wananchi 'Peoples Palace' lililoko Forodhani.

Rais Mwinyi alisema ujenzi huo una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya Zanzibar huku akisisitiza kuna kila sababu ya kuzitunza nyumba za Mji Mkongwe wa Zanzibar kutokana na haiba yake.

Alisema uwapo wa Kampuni ya Ndege ya Oman inayofanya safari kati ya Zanzibar na Oman, kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha biashara kati ya pande mbili hizo huku akisisitiza Zanzibar ina bidhaa nyingi zenye soko Oman.

Balozi Mdogo wa Oman, Alsinawi, alisema Serikali ya Oman iko tayari kuendeleza ushirikiano wake na Zanzibar ikiwa ni pamoja na kuiunga mkono katika kuimarisha miradi yake ya maendeleo.

Alisema Serikali ya Oman inatambua uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Oman na Zanzibar pamoja na watu wake, hivyo nchi yake itaimarisha zaidi uhusiano huo.

Balozi huyo alisema Oman inathamini uhusiano na ushirikiano huo wa kihistoria uliopo na inatambua juhudi kubwa anazozichukua Rais Mwinyi kuiletea Zanzibar maendeleo, hivyo haina budi kumuunga mkono ili kufikia lengo lake alilolikusudia.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAWRENCE SALVATORY ANATORY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 561 CHK**,chasis namba **NCP610071353**,engine namba **INZB111118**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/URA/R-B/350790/2021**

116358502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IMANI LODENI MNYIKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MTSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 777 AWG** ,chasisi namba **FK629M530018**,engine namba **6D17880811**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MKB/RB/2040/2021**

116359002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MCA/63)**

**MAHAKAMA YA MWANZO MULEBA MJINI**

**TALAKA MADAI NAMBA 9/2021**

Bwana **Liston Onesmo** unatakiwa mbele ya mahakama hii siku ya Jumatatu tarehe **19/Julai/2021 saa 7 asubuhi** kwa ajili ya shauri lililopo mbele ya Mahakama hii lililofunguliwa na Leath Cyliacus. Ukifika usiondoke bila ruhusa ya Mahakama na ukipuuza wito huu itatolewa hati ya kukulazimisha kuhudhuria.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii

Kuitwa shaurini hii kwa maombi ya :- LEATH CYLIACUS

116358802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ...MJINI TANGA............**

**Usimamizi wa Mirathi................9/2021........................**

**Ombi la......MOHAMED SALIM AMRI... kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya marehemu ...ALI SALIM AMRI...**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyu wanaalikwa Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 19/7/2021 kabla huyo mwomwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 14/7/2021.

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

116359502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA TARAKA NAMBA: 68/2021**
**MADAI : ESTER ELIAS SENG`UNDA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: ANJELUS LEONARD NGUYA**
**KWA: ANJELUS LEONARD NGUYA**
**OMBI LA MDAI**
**ESTER ELIAS SENG`UNDA**
**MADAI YA : TARAKA , UANGALIZI WA MTOTO NA MATUNZO YA MTOTO MMOJA**

Unatakiwa kuhudhuria hapa mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa . Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 23 mwezi 07 mwaka 2021 saa 2:30 Asubuhi.

Angalia kama *kuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 14 mwezi 07 mwaka 2021

**HAKIMU**
**MAHAKA MA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

116359302




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Fawzia mwanamke pekee mgombea urais Somalia



**Mogadishu,** SOMALIA

MBUNGE mwanamke ametangaza kugombea wadhifa wa urais katika uchaguzi mkuu wa rais ujao.

Fawzia Yusuf Adam anakuwa mwanamke pekee kati ya wagombea 10, ambao wanatarajiwa kupigiwa kura Oktoba 10.

Adam ni msaidizi wa zamani wa waziri mkuu na aliwahi kuwa waziri wa mambo ya nje.

Atawania dhidi ya kiongozi aliyeko madarakani Mohamed Abdullahi Mohamed, anayejulikana kwa jina la utani la Farmajo na wengine wawili waliowahi kuwa marais na wengineo.

Adam anasema atapumua na kuweka Somalia mpya.

Viongozi wa Somalia wamekubaliana kuwa na uchaguzi mwezi Oktoba baada ya kusubiri kwa muda.

Uchaguzi ulicheleweshwa kutokana na baadhi ya viongozi kushindwa kushiriki katika mazungumzo ya uchaguzi ambapo walisababisha maandamano kutokea.

Uchaguzi wa Somalia huwa unafanyika na wawakilishi wa koo kabla ya siku ya kupiga kura.

**BBC**

# Vifo vyafikia 72 Afrika Kusini

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

WATU 72 wamepoteza maisha Afrika Kusini baada ya ghasia kuendelea kushuhudiwa kati ya wafuasi wa rais wa zamani Jacob Zuma na maofisa wa usalama.

Maduka na maghala yameporwa kwa siku ya tano mfululizo, licha ya hatua ya Rais Cyril Ramaphosa kupeleka wanajeshi 2000 mitaani ili kuzima na kudhibiti hali.

Wafuasi wa Zuma ambaye amefungwa jela, wamekuwa wakiandamana katika miji mbalimbali, kushinikiza kuachiliwa huru kwa kiongozi wao, ikiwamo jiji la Johannesburg na mkoa wa KwaZulu-Natal.

Maofisa wachache wa usalama walionekana karibu na maduka yanayoporwa na wananchi wa taifa hilo, huku idadi ya vifo ikiendelea kupanda, hasa kutokana na watu kukanyagana.

Watu wengine zaidi ya 1,200 na wamekamatwa katika machafuko hayo.

Wafuasi wa Zuma wanasema wataendelea kuandamana hadi kiongozi wao aliyefungwa jela miezi 15 atakapoachiliwa huru.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN), Afrika Kusini, ilielezea wasiwasi kwamba maandamano hayo ya vurugu yametatiza usafiri kwa wafanyakazi, wahudumu wa afya na pia yanasababisha upungufu wa vyakula, dawa na bidhaa nyingine muhimu.

Kwenye taarifa, UN, ilisema hali iliyoko inazidisha hali duni za kijamii na kiuchumi ambazo zimekuwapo kutokana na ukosefu wa nafasi za ajira, umaskini na ukosefu wa usawa nchini humo.

Jumanne, wiki hii, wanajeshi walipelekwa mitaani kuwasaidia polisi ambao walishalemewa kujaribu kudhibiti machafuko.

Mamlaka ya mashtaka ya umma ilisema itawaadhibu wale watakaokamatwa wakipora na kuharibu mali. Lakini onyo hilo halijazuia uporaji au uharibifu unaoshuhudiwa.

**KIFUNGO**

Jacob Zuma ambaye ana umri wa miaka 79 kwa sasa, ni rais wa zamani wa Afrika Kusini, mpiganaji wa zamani katika vita dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Aliwahi kufungwa jela miaka 10 katika gereza lenye sifa mbaya kisiwani Robben karibu na mji wa Capetown.

Zuma alianza kutumikia adhabu ya kifungo cha miezi 15 jela baada ya kulala korokoroni wiki iliyopita licha ya maandamano ya kupinga hukumu hiyo kutoka kwa wafuasi wake.

Baada ya siku kadhaa za maigizo na chenga za kutaka kuikwepa adhabu hiyo, alianza kutumikia kifungo cha miezi 15 jela baada ya kupelekwa katika gereza la EstCourt lililoko katika jimbo anakotoka la KwaZulu- Natal.

Zuma ambaye ni mfungwa wa zamani wa utawala wa ubaguzi wa rangi, alizusha taharuki nchini humo baada ya kujaribu hatua za kisheria za kuepukana na adhabu hiyo, kwa mara nyingine amejikuta mfungwa.

Hii ni mara ya kwanza kwa rais wa zamani kufungwa katika enzi za baada ya utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini. Singabakhe Nxumalo ni msemaji wa idara ya magereza.

"Zuma aliwasili saa saba usiku, walimleta kwetu lakini sasa tunapaswa kuchukua jukumu na ninahitaji kuwahakikishia kuwa amezuiliwa katika ulinzi salama na pia tunapaswa kujibu mahitaji yake maalumu ikiwa kuna lolote limetambuliwa."

Hukumu hiyo iliyotolewa dhidi ya Zuma na Mahakama ya Katiba ilitokana na kuwapuuza wachunguzi wanaofuatilia madai ya ufisadi, pia iliiandika historia barani Afrika kwa kumfunga mkuu wa zamani wa nchi kwa kukataa kujibu mashitaka ya rushwa.

Kiongozi wa upinzani wa Chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) Afrika Kusini, Julius Malema jana alizuiwa kwa muda kuandika katika akaunti yake ya Tweeter kwa kukiuka miongozo ya mtandao huo, vyombo vya habari vya ndani viliripoti.

Malema alitishia kuhamasisha wafuasi wake kushiriki katika vurugu kubwa ambazo zinapinga kufungwa kwa Zuma, zilizoanzia KwaZulu-Natal na jimbo la Gauteng.

Mbuyiseni Ndlozi, mbunge na mwanachama wa chama cha EFF, Jumanne wiki hii, aliweka picha ya ujumbe ambao unaonyesha Malema amezuiwa kwa muda kuandika kwenye twitter.

Malema amezuiliwa kuandika na kushiriki ujumbe wa wengine kwenye akaunti yake ya twitter kwa muda wa takribani saa 12.

**RFI/DW/ BBC/REUTERS**




Waandamanaji nchini Afrika Kusini wakiingia kwenye maduka na kupora baadhi ya vitu hali iliyosababisha vurugu na vifo vya watu 72 hadi jana. **PICHA: BBC**

# Idadi wahamiaji waliokufa maji yaongezeka 2021

**Grand-Saconnex,** USWISI

KWA kipindi cha miezi mitatu ya kwanza ya mwaka huu wa 2021, watu wasiopungua 1,146 walikufa maji baharini wakijaribu kuvuka Bahari ya Mediterranean kuingia Ulaya, kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM).

Idadi ya wahamiaji waliokufa maji baharini wakijaribu kuingia Ulaya imeongezeka zaidi ya mara mbili mwaka huu, IOM limesema jana, huku likitoa wito kwa mataifa kuchukua hatua za haraka.Kulingana na takwimu zilizotolewa na IOM katika ripoti mpya, watu wasiopungua 1,146 walikufa maji baharini wakijaribu kuingia Ulaya katika kipindi cha miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2021.

Mwaka jana, watu 513 walikufa maji kwa kipindi kama hicho na watu 674 walikufa maji mwaka 2019.

"Mashirika yanayotoa msaada kwa shughuli za uokoaji wa raia yameendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali, na boti zao nyingi zimekwama katika bandari za Ulaya kutokana na kesi za jinai dhidi ya wafanyakazi wa boti hizo." Inabainisha ripoti hiyo.

IOM pia inabainisha kuwa ongezeko la vifo linakuja wakati vizuizi vya boti zinazobeba wahamiaji kutoka pwani ya Afrika Kaskazini, vinaongezeka.

**RFI**



# Laporta: Tumefikia pazuri na Messi

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amesema wanakaribia kufikia makubaliano ya mkataba mpya na nyota wao, Lionel Messi.

Kwa sasa Messi, mwenye umri wa miaka 34 yupo huru baada ya pande hizo mbili kushindwa kukubaliana vipengele kadhaa kabla ya mkataba wake wa awali uliomalizika Juni 30, mwaka huu, ingawa majadiliano yanaendelea.

Licha ya kutofikiwa makubaliano, Laporta ana imani kuwa Messi atatia saini mkataba na kujifunga tena Barca kwa ajili ya hatima yake.

Akiwa amefanikiwa kutwaa ubingwa wake wa kwanza wa kimataifa na Timu ya Taifa ya Argentina baada ya kushinda fainali ya Copa America dhidi ya Brazil, Messi atahamishia fikra zake kwa klabu ya baadaye ambayo bado haijajulikana.

Wakati Barcelona inakabiliwa na matatizo ya kifedha sasa, Messi amekuwa kimya kuhusu hatima yake.

Hivi karibuni kocha wa Barcelona, Ronald Koeman amekiri Messi yuko katika mkanganyiko, lakini alielezea imani yake kwamba Laporta ataweza kupata ufumbuzi.

"Wakati tatizo linapokuwa halijapatiwa ufumbuzi, unakuwa kwenye wasiwasi," Koeman ameliambia gazeti la Marca la Hispania.



# Abramovich amfungia kazi Haaland

**LONDON,** England

BILIONEA Roman Abramovich ameipatia klabu ya Chelsea fedha kiasi cha dola milioni 150 kwenda Ujerumani kumnasa mshambuliaji nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kwa ajili ya msimu ujao.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akiwindwa na klabu kubwa za Ulaya msimu huu zikiwamo Manchester City na Real Madrid.

Haaland ambaye alifunga mabao 41 katika mechi 41 za msimu uliopita katika klabu ya Borussia Dortmund atafuata nyayo za Jadon Sancho wa England kuondoka Dortmund iwapo ataihama klabu hiyo msimu huu.

Sancho anatajwa amejiunga na Manchester United kwa dau la dola milioni 73 na mapema juzi Jumatatu alifanyiwa vipimo vya afya.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild la Ujerumani Abramovich ametoa fedha hizo kwa ajili ya Chelsea kumsajili Haaland msimu huu, lakini atahitajika kuwaondoa baadhi ya washambuliaji nyota ili kukamilisha dili kwa wakati.

Ripoti zimedai washambuliaji Callum Hudson-Odoi, Tammy Abraham na Hakim Ziyech ni baadhi ya wachezaji wanaokabiliwa na panga hapo Stamford Bridge iwapo watashinda kinyang'anyiro cha kumsajili Haaland



# Rashford kupasuliwa bega

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford ataukosa mwanzo wa msimu huu mpya wa Ligi Kuu England kwa kuamua kufanyiwa operesheni ya bega baada ya michuano ya Euro 2020, kwa mujibu wa ripoti.

Fowadi huyo wa Manchester United, ambaye alikosa penalti wakati England ikifungwa na Italia 3-2 kwenye fainali ya Euro 2020 Jumapili kabla ya kukumbwa na ubaguzi kwenye mitandao wa kijamii, atakuwa nje ya dimba kwa karibia wiki 12, hadi Oktoba, mwaka huu.

BBC Sport imeripoti kuwa Rashford alifayiwa vipimo vya bega lake Jumanne, ambapo vilionyesha kwamba ameumia na anahitaji kufanyiwa upasuaji.

Hata hivyo, operesheni hiyo haitafanyika sasa ni hadi mwishoni wa mwezi huu.

United itaanza msimu mpya wa Ligi Kuu England 2021-22 kwa mchezo dhidi ya Leeds United ifikapo Agosti 14, mwaka huu.

Rashford alikuwa na matatizo ya bega kwa kipindi chote cha msimu wa 2020-21 na iliripotiwa awali kwamba, atafanyia upasuaji baada ya michuano ya Euro.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alifunga mabao 21 katika mechi 57 kwenye mashindano yote kwa mashetani wekundu hao msimu uliopita.

Hakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi cha England kwenye michuano ya Euro 2020, kwani alitokea benchi mara tano.

HABARI MICHEZO



# Mourinho ateua maskauti wa usajili

**ROME,** Italia

KOCHA Mourinho amewateua maskauti watano katika klabu ya Roma kutoka maeneo tofauti barani Ulaya akiwamo mkuu wa kuvumbua vipaji wa Leicester City, Jose Fontes, ripoti zimesema.

Kocha huyo raia wa Ureno alitangazwa kuwa kocha mpya wa Roma mwishoni mwa Mei na amewasili katika mji mkuu wa Italia, Rome wiki iliyopita wakati mkataba wake kwenye klabu hiyo inayojulikana kama Giallorossi umeanza Julai Mosi, mwaka huu.

Miongoni mwa majina mapya ya wasaidizi wake ni skauti wa kireno, Fontes ambaye alisaidia usajili wa Harry Maguire, Caglar Soyuncu na Youri Tielemans kwenye klabu ya Leicester.

Kwa mujibu wa Corriere dello Sport, Mourinho pia amemteua skauti wa AC Milan Enrico Paresce, skauti wa zamani wa vipaji wa Juventus na Inter Milan, Mauro Leo, mchambuzi wa zamani wa Leverkusen, Javier Weimar na mtaalamu ambaye ni mchezaji wa zamani wa Roma, Alessio Scarchilli.

Maskauti hao watamsaidia mkurugenzi wa michezo wa Roma, Tiago Pinto kufanya vyema majukumu yake.

Mourinho anakusanya kikosi chenye uwezo wa kushindania nafasi nne za juu katika Ligi ya Kuu Italia, Serie A baada ya Roma kumaliza ikiwa nafasi ya saba msimu uliopita.

## Liverpool yafikia pazuri kwa Niguez

**LIVERPOOL,** England



MCHAKATO wa Liverpool kumnasa, Saul Niguez unatajwa kuwa upo kwenye hatua nzuri baada ya Atletico Madrid kumleta Rodrigo De Paul kama mbadala wa kiungo huyo.

Liverpool wanasemekana kuongoza mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye alipambana kuanza mara kwa mara chini ya Diego Simeone kwenye msimu wa 2020-21.

Saul bado ana miaka mingine mitano ya kuendelea kuwako klabuni hapo kwa mujibu wa kandarasi iliyosainiwa 2017, lakini mchezaji huyo wa Atletico anaaminika yuko mbioni kuondoka msimu huu wa joto.

Klabu kadhaa kubwa barani Ulaya zimekuwa zikipigana vikumbo kuwania saini ya nyota huyo.

Lakini sasa Liverpool ndio wenye nafasi nzuri zaidi ya kupata huduma yake, kwani mchezaji mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kuhamia kwa miamba hao wa Ligi Kuu England.

## Inter wavunja mkataba na Mario



**MILAN,** Italia

KLABU ya Inter Milan imekubali kukatisha mkataba na kiungo wa kimataifa wa Ureno, Joao Mario kwa ridhaa ya pande zote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alijiunga na Inter kutoka Sporting kwa pauni milioni 35 mwaka 2016 baada ya kushinda Euro na Ureno lakini alipambana kuingia kwenye kikosi cha kwanza, akitumia wakati wake mwingi nje kwa mkopo.

Mario alikuwa na msimu wa mkopo na West Ham United mwaka 2018, kabla ya kutua Lokomotiv Moscow na Sporting.

"Asante sana Inter. Kila la kheri kwa siku zijazo," Joao Mario aliandika katika ujumbe mfupi kwenye Twitter.

Mario alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshinda taji na Sporting msimu uliopita wakati klabu ya Ureno ilimaliza miaka 19 ya ukame wa kulikosa Kombe la Ligi Kuu Ureno, Primeira Liga.

Mshindi huyo wa Euro 2016 alicheza mechi 69 tu na Nerazzurri wakati wa miaka yake mitano na klabu hiyo na alikuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa.

Anatarajiwa kujiunga na Benfica lakini sehemu ya mkopo wake na Sporting ilimzuia kujiunga na klabu nyingine ya Ureno isipokuwa Inter ililipia ada kubwa, na hivyo kuamua kuachana naye.

Inafahamika Benfica walikuwa tayari kulipa pauni milioni 6.4 kwa Mario, ambaye sasa ni mchezaji huru.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI MBIONI KUJIUNGA NA MADRID

●●● Tayari Bayern Munich imeshaanza mchakato wa kuzungumza na Gakpo ili kuziba pengo…

**MUNICH,** Ujerumani

MSHAMBULIAJI nyota wa Bayern Munich, Robert Lewandowski anaangalia uwezekano wa kuhamia Real Madrid huku klabu hiyo ya Ujerumani ikitafuta mbadala wake kwa ajili ya msimu mpya.

Mkataba wa Lewandowski mwenye umri wa miaka 32 katika klabu ya Bayern Munich unafikia ukingoni ifikapo mwaka 2023 na mabingwa hao wa Ujerumani wana wasiwasi ataomba kuondoka mwaka ujao wakati ada ya uhamisho itakapokuwa imepungua.

Lewandowski alifunga mabao 41 msimu uliopita wa Bundesliga akivunja rekodi ya Gerald Muller ya mabao 40 katika msimu mmoja wa ligi.

**Kwa mujibu wa mtandao wa habari za michezo, AS, wa Hispania Bayern inataka kuziba pengo la Lewandowski kwa kumsajili chipukizi wa PSV Eindhoven ya Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 22.**

Licha ya Gakpo kucheza nafasi ya winga bosi mpya wa Bayern, Julian Nagelsmann anataka kumtumia chipukizi huyo katika nafasi ya mshambuliaji namba tisa kama alivyomtumia Dani Olmo wakati akiwa kocha wa RB Leipzig.

Wakati huo huo Roma wamekamilisha mchakato wa kumsajili golikipa Mreno Rui Patricio kutoka Wolves.

Taarifa rasmi iliyotolewa Jumanne jioni na klabu hiyo ya Ligi Kuu England imethibitisha kumuuza mchezaji huyo kwa dau la pauni milioni 9.8.

Patricio (33), anakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa chini ya Jose Mourinho tangu alipojiunga na Roma Mei mwaka huu akitokea Tottenham.

Golikipa huyo alijiunga na Wolves mwaka 2018 baada ya kuomba kuondoka katika kikosi cha Sporting kufuatia mashabiki wa klabu hiyo ya jiji la Lisbon kushambuliwa na mabomu kwenye viwanja vya mazoezi.

## KWA UFUPI

### GRIEZMANN NJIA MOJA
CHELSEA wanafanya mipango ya kumsajili Mfaransa Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30, kwa mkopo kutoka Barcelona. ***(Daily Express)***

### HALAAND ANUKIA CHELSEA
CHELSEA wanakabiliwa na "misheni isiyowezekana" wakati wanazidisha juhudi zao za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, msimu huu wa majira ya joto. ***(Sky Sports)***

### INGS ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imemfanya mshambuliaji wa Southampton, Danny Ings (28), kuwa kipaumbele chao wakiamini atacheza nafasi ya ushambuliaji sambamba na Harry Kane, wanayetaka kumbakisha. ***(Telegraph)***

### NEVES KUTUA ARSENAL
ARSENAL wana mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves kwa kitita cha pauni milioni 35. ***(Sun)***

### LOCATELLI AITAKA JUVE
MCHEZAJI anayelengwa na Arsenal, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 23 ambaye anakipiga katika klabu ya Sassuolo ya Italia, amekaribisha nia ya Juventus kumsajili.***( AS)***

### SPURS, UNITED VITANI
TOTTENHAM Hotspur na Manchester United zinataka kumsajili mlinzi wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 23, ambaye amefika nusu ya muda wa mkataba wake na Atlanta anakocheza kwa mkopo akitokea Juventus. ***(Calciomercato)***

### DONNARUMMA SAFI PSG
KLABU ya Paris St-Germain inajiandaa kutangaza usajili wa mlinda mlango wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma mwenye umri wa miaka 22. ***(Daily Express)***

### GREALISH AONYWA
KIUNGO wa kati wa Aston Villa na England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 25, ameonywa dhidi ya kuhamia kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City. ***(Daily Mirror)***

### TOWNSEND ATAFUTA TIMU
WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Andros Townsend mwenye umri wa miaka 29, anatafuta klabu mpya baada ya kuona kuna uwezekano mdogo wa kuongezewa mkataba na Crystal Palace. ***(Evening Standard)***

### CHALOBAH SOKONI
KLABU ya Brentford imejiunga na West Brom katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea, Trevoh Chalobah. Klabu ya Lorient ya nchini Ufaransa pia inamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Express & Star)***

### ANDERSON ATUA LAZIO
KIUNGO wa kati wa West Ham, Felipe Anderson mwenye umri wa miaka 28, yuko Italia kwa ajili ya kukamilisha usajili na Lazio, ikiwa ni miaka mitatu baada ya kuondoka kwenye klabu hiyo na kujiunga na wagonga nyundo hao wa London. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS KUONGEZA 'MAKALI' KUELEKEA CECAFA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema kikosi chake hakijaathirika na uamuzi wa kusogezwa mbele kwa mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika ya Wanawake kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), ambayo yalitarajiwa kufanyika kuanzia kesho nchini Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mgosi alisema anaamini mabadiliko hayo ya tarehe hayakufanywa kwa makosa na anaamini muda uliopo ataendelea kukiimarisha kikosi chake ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Mgosi alisema ataendelea kuimarisha wachezaji wake kwa kufanya programu mbalimbali na hatimaye kwenda katika mashindano hayo wakiwa imara zaidi.

"Hatutaathirika na kusogezwa mbele kwa michuano hiyo, tumejiandaa vizuri na baada ya mabadiliko hayo ya kuanza kwa mashindano tumewapa mapumziko ya siku nne wachezaji wetu, tutaingia tena kambini Jumapili ili kuendelea na mazoezi," alisema Mgosi.

Aliongeza kikosi chake kitaendelea kuweka kambi hapa jijini na anamshukuru Mungu hana majeruhi kwenye timu hiyo.

"Awali tulikuwa tunafikiria tutoke kwenda mkoa wa karibu kulingana na hali ya hewa ya baridi ya Kenya, baada ya mabadiliko haya tutabaki Dar es Salaam tukiendelea kujifua, tunataka kwenda huko tukiwa imara zaidi kwa ajili ya kuiletea nchi heshima," alisema Mgosi.

Alisema wanaendelea pia kuwafuatilia wapinzani wao kwa kutizama video za mechi mbalimbali walizocheza kabla ya kuelekea kwenye kinyang'anyiro hicho cha kusaka timu nane zitakazokwenda Misri katika fainali hizo za kwanza.

Simba Queens imepangwa Kundi A pamoja na Lady Doves WFC ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Uganda na PVP FC ya Burundi wakati Kundi B linaundwa na New Generation Queens ya Zanzibar, Yel Joint Stars (Sudan Kusini) na timu ya Benki ya Biashara ya Ethiopia huku FAD ya Djibout na Vihiga Queens ya Kenya zikisalia katika Kundi C baada ya Scandinavia ya Rwanda kujiondoa katika mashindano hayo.

Wakati huo huo, Mgosi ameweka wazi timu hiyo haijamsajili straika chipukizi, Violeth Masele (13), ambaye alionekana katika mchezo wa kirafiki waliocheza dhidi ya Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ambao ulimalizika kwa Simba Queens kuchapwa mabao 2-1.

Mgosi alisema alimpa mchezaji huyo ambaye ni mwanafunzi kuonyesha uwezo wake lakini akitarajiwa kwenda kuitangaza Simba Queens atakaporejea masomoni Marekani.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Opa Clement (kushoto), akifunga bao katika mechi ya kirafiki dhidi ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Twiga Stars ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Biashara United nguvu zote CAF

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Biashara United umesema unatarajia kufanya kikao cha tathmini ya kikosi chao cha msimu huu na kupanga mikakati ya kukiboresha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso alisema tayari wamekabidhiwa ripoti ya ufundi kutoka kwa kocha wao kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao.

Mataso alisema baada ya mchezo wao wa leo dhidi ya Tanzania Prisons, viongozi watakutana na kuangalia mwenendo mzima wa timu hiyo kwa msimu huu ambao utawapa mwongozo kuelekea katika msimu mpya ambao unatarajiwa kuwa na ushindani zaidi.

"Tunakutana ili kujadili mambo mbalimbali, hapa kati kuna mambo mengi yalitokea tukiwa mwishoni mwa msimu ikiwamo kumtangaza Kocha mpya, Patrick Odhiambo Okumu ambaye amechukuwa nafasi ya Francis Baraza aliyeondoka."

"Odhiambo amekuta timu imesajili na sasa anatoa mapendekezo yake na baada ya mechi ya kesho (leo), viongozi tutapanga mikakati yetu imara kwa ajili msimu ujao wa ligi," alisema Mataso.

Aliongeza wanahitaji kufanya vizuri katika michezo miwili iliyobakia ili kujihakikishia kumaliza msimu huu katika nafasi ya nne na hatimaye kupata tiketi ya kushiriki kwenye michuano ya kimataifa.

Biashara United iko katika nafasi ya nne ikiwa na pointi 49 na leo watashuka dimbani ugenini kuwakabili Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa.

# Msimamo watwaa Kombe la Ng'ombe

**Na Beatrice Shayo**

TIMU ya Msimamo FC kutoka Kata ya Mnyamani Buguruni imeibuka mshindi wa mashindano ya kuwania Kombe la Ng'ombe baada ya kuifunga Machafu Love mabao 2-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sinai jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Mashindano hayo yaliandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la CAFLO.

Kwa ushindi huo, Msimamo FC wamepata zawadi ya ng'ombe mmoja mwenye thamani ya Sh. milioni moja wakati Machafu Love ambao wanatoka Kata ya Mnyamani walipewa zawadiwa mbuzi mwenye thamani ya Sh. 200,000.

Akizungumza wakati wa fainali hizo, Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambaye alikuwa mgeni rasmi katika fainali hizo, Saad Khimj, aliwataka vijana wote walioshiriki katika mashindano hayo kuwa mabalozi kwa kuendelea kuelimisha jamii juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

Khimj alisema michezo ni afya na mashindano hayo yamefanyika ili kuhamasisha vijana kuwa na tabia ya kucheki afya zao mara kwa mara.

Naye Mwenyekiti wa CAFLO, Mariam Mlugu alisema wanatekeleza malengo ya mradi ya kudhibiti maambukizi ya VVU ambapo mashindano hayo yalishirikisha timu 16 kutoka katika Kata za Vingunguti, Mnyamani, Buguruni, Tabata na Kipawa.

"Mradi huu umewalenga vijana wenye umri wa kuanzia miaka 14 hadi 25 waliopo katika kata hizi kwa sababu ndiyo kundi linaloonekana kuwa katika hatari kubwa ya kupata maambukizi ya VVU ikilinganishwa na makundi mengine," alisema Mlugu.

Alisema pia wamefanikiwa kuunda na kuendeleza majukwaa ya vijana hususani wasichana kwa lengo la kuwawezesha kupata elimu na mbinu ya kujikinga na VVU na kuwahamasisha kushiriki katika shughuli za kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

"Tunaamini kwamba vijana wakipata fursa ya kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi ni njia mojawapo ya kuwawezesha kujikinga na maambukizi ya VVU," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kupitia mradi huo pia waliendesha midahalo kwa wanafunzi wa shule za sekondari na mpira wa pete kwa wasichana ili kuwaelimisha na kuhamasisha kujikinga na maambukizi ya VVU.

Michezo

Alhamisi Julai 15, 2021

Nipashe



LEWANDOWSKI MBIONI KUJIUNGA NA MADRID

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Azam FC, Mpiana Mozizi (kushoto) na beki wa timu hiyo, Bruce Kangwa wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya mabingwa Simba, itakayochezwa leo usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam. PICHA: MTANDAO

## NIYONZIMA AAHIDI KURUDI TENA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Yanga, Haruna Niyonzima ambaye leo ataagwa na klabu yake baada ya kuitumikia kwa muda wa miaka tisa, amesema huenda akarejea tena nchini Tanzania kama siyo mchezaji basi anaweza kurudi akiwa kocha.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Niyonzima raia wa Rwanda amesema kitendo cha kuagwa kwa heshima kimemfanya ajisikie vizuri na kuona amethaminiwa na klabu yake hiyo.

"Naishukuru sana klabu yangu, nawashukuru sana wanachama na mashabiki wote wa Yanga, tumekuwa na kipindi kizuri tukiwa wote, lakini mimi maisha yangu ni mpira, kwa hivyo nitaendelea kuwepo kwenye tasnia hii hii ya soka, na naweza kurejea tena hapa nchini, kama siyo mchezaji, basi naweza kurudi kama kocha," alisema mchezaji huyo ambaye alianza kusomea ukocha tangu akiwa na Simba.

Kuhusu kitendo chake cha kuondoka kwenye klabu hiyo na kujiunga na Simba, Niyonzima alisema hiyo ilikuwa ni moja kati ya harakati zake za kutafuta maisha na si vinginevyo.

"Wanachama na mashabiki wajue haya ni maisha na ndiyo yanayonifanya niendeshe familia, kwa hiyo niliondoka kwa sababu huu mpira ni kazi, leo unaweza ukawa nayo kesho huna, lakini kujijenga na maisha ya baadaye. Lakini nashukuru baadaye mashabiki wengi walielewa hilo na kasababisha nirudi tena kwenye klabu hii ya Yanga," alisema kiungo huyo.

Mchezaji huyo anaagwa leo wakati ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ikicheza dhidi ya Ihefu SC kwenye Uwanja wa Bemjamin Mkapa jijini. Niyonzima anaondoka Yanga akiwa ameichezea kwa miaka tisa, kwa vipindi viwili tofauti, alijiunga na klabu hiyo ya Jangwani mwaka 2011 akitokea APR ya Rwanda na kuichezea hadi 2017, alipohamia kwenye klabu ya Simba na kuichezea kwa miaka miwili hadi 2019.

# Ni vita ya kusalia, heshima Ligi Kuu

## ●●● Coastal Union, Gwambina zenyewe ziko 'roho mkononi' katika mapambano....

**Adam Fungamwango**

MECHI za raundi ya 33 ya Ligi Kuu Tanzania Bara zitachezwa leo kwenye viwanja mbalimbali nchini, lakini macho na masikio ya mashabiki wa soka nchini yamehamia kuangalia ni timu gani zitakazosalia, kushuka daraja au zitakazokwenda kucheza mechi za mtoano.

Timu zote 18 zitakuwa viwanjani kusaka pointi tatu, huku nyingine zikikamilisha ratiba ya msimu huu wa 2020/21.

Mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 Simba wao watakuwa wanakamilisha ratiba yao ugenini kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kucheza na wenyeji Azam FC ambao wanahitaji kumaliza msimu kwa heshima.

Mechi nyingine itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ambapo Yanga itawakaribisha Ihefu ya jijini Mbeya.

Ni mechi ambayo Yanga inahitaji pointi moja tu ili kuwa na uhakika zaidi wa kumaliza nafasi ya pili, kwani ikifikisha pointi 71, hakuna timu yoyote ya chini yake itakayofikisha pointi hizo.

Hata hivyo ni mechi muhimu sana kwa Ihefu yenye pointi 35, na nafasi ya 15, kwani inahitaji pointi tatu ili kuondoka katika eneo la hatari na kwenye Uwanja wa Uhuru, KMC itaikaribisha JKT Tanzania. KMC inaingia uwanjani ni kama kulinda heshima tu, kwani ipo salama ikiwa nafasi ya sita kwa pointi 42, lakini hali ni mbaya kwa JKT Tanzania ambayo ina pointi 36, ikiwa kwenye nafasi ya 14.

Mjini Sumbawanga kwenye Uwanja wa Nelson, Tanzania Prisons itacheza dhidi ya Biashara United. Prisons iko eneo salama ikiwa kwenye nafasi ya saba baada ya kujikusanyia pointi 42, inacheza na Biashara United ambao inahitaji pointi moja tu ili ijihakikishie kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

Timu hiyo yenye pointi 49, inahitaji pointi moja ifikishe 50, na kuifanya Namungo FC yenye pointi 43 kushindwa kufikia idadi hiyo kwani itafikisha pointi 49 tu ikishinda mechi mbili zilizobakia. Moja ya mechi ambayo itaangaliwa sana ni kati ya Coastal Union dhidi ya Mwadui FC, kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

**Coastal ikiwa maji ya shingo, kwenye nafasi ya 17 na pointi zake 34, inahitaji ushindi wa lazima, kwani matokeo mengine zaidi ya hapo, itakuwa imeshuka daraja.**

Mwadui, timu pekee ambayo imeshashuka daraja, inaweza kuwa ni sawa na mfa maji, ambaye anataka kufa na mtu.

Dodoma Jiji, yenyewe itakuwa nyumbani ikiikaribisha Mtibwa Sugar. Ingawa haipo kwenye hatari sana, lakini timu hiyo inahitaji ushindi angalau wa mechi moja kati ya mbili zilizosalia ili kujihakikishia kusalia moja kwa moja kwenye Ligi Kuu, vinginevyo inaweza kwenda kucheza mechi za mchujo. Katika msimamo wa ligi, Mtibwa Sugar yenye pointi 38, iko kwenye nafasi ya tisa, hata hivyo inacheza na timu inayotapatapa kutaka kujinasua kwenye hatari ya kushuka daraja huku Mbeya City wakiwavaa Gwambina iliyokalia kuti kavu.

Polisi Tanzania itacheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ambayo maafande watakuwa wakihitaji pointi ili kuepuka kucheza mechi za mtoano, huku Kagera Sugar yenye pointi 37 ikiwa kwenye nafasi ya 12, ikitaka ushindi ili isalie Ligi Kuu Bara.

Vita nyingine itakuwa kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani, Ruvu Shooting yenye pointi 38, ikihitaji ushindi dhidi ya Namungo ili kuhakikisha usalama wake kutocheza mechi za mchujo, lakini Namungo FC ikihitaji ushindi pia ili kuifukuzia nafasi ya nne, kama Biashara United itapoteza mechi mbili zilizobaki.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042